



South Dakota
IDARA YA ELIMU
Mafunzo. Uongozi. Huduma.

Imehaririwa 2020

South Dakota

Mchakato na Haki za Wazazi



Mojawapo wa jukumu muhimu la mzazi anapomkuza mtoto wake ni kumpa elimu. Wazazi wanaweza kuchagua kuwapa watoto wao huduma za **Elimu kwa watu wenye ulemavu**, kwa wanafunzi wa miaka kati ya 3 hadi 21 ambao wanatatizika kusoma kwa sababu ya ulemavu. Ukigundua kuwa mtoto wako anatatizika kimasomo, kuchangamana na watu au kihisia unahimizwa kushirikiana na wahudumu wa shule kubaini mbinu za kumsaidia. Si kila mtoto anayetatizika shuleni anastahiki kupata huduma za elimu kwa watu walio na ulemavu.

Madhumuni ya hati hii ni kukupa maelezo muhimu na ya msingi kuhusu haki zako kama mzazi wa **mtoto aliye na ulemavu** katika eneo la South Dakota. Tafadhali isome kwa umakinifu. Ikiwa una maswali au unahitaji usaidizi wa kuelewa kanuni za elimu kwa watoto walio na ulemavu katika Jimbo, wasiliana na shirika lolote kati ya mashirika yaliyoorodheshwa mwishoni mwa hati hii, mtawala wa wilaya ya shule yako au mwakilishi wake.

Sheria ya Elimu kwa watu walio na Ulemavu (IDEA) ni sheria ya shirikisho inayohitaji shule kuwa na huduma za elimu kwa watu walio na ulemavu na kubaini utaratibu ambao shule sharti ifuate. Sheria ya jimbo pia ina masharti ya kuwapa elimu wanafunzi wenye ulemavu. Ikiwa wewe ni mzazi wa mtoto aliye na ulemavu uliorodheshwa katika IDEA, kijitabu hiki ni hati ya utaratibu wa kukulinda na kinakuelezea vigezo na masharti ya elimu kwa watoto walio na ulemavu.

**** Unaweza kupata maneno yote yenye rangi nzito katika hati hii kwenye ukurasa wa ufupisho na ufafanuzi mwishoni.**

Anwani ya shule ya Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu

Wilaya: Tafadhali ongeza maelezo yafuatayo kwenye kisanduku hiki.

Anwani ya Wilaya:

Nambari ya Simu:

Anwani ya Barua pepe:

Jedwali la Yaliyomo

MAELEZO YA KIJUMLA	5
Upatikanaji wa Notisi ya Ulinzi wa Utaratibu	5
Idhini ya Mzazi	5
Idhini ya Tathmini ya Awali	6
Idhini ya Huduma	7
Idhini ya Kutathmini Upya.....	8
Masharti mengine ya idhini	9
Ilani ya Kuandikwa Mapema.....	9
Tathmini Huru ya Elimu (IEE)	10
REKODI ZA ELIMU.....	12
Usalama wa maelezo na ufikiaji wa rekodi za elimu	12
Ilani kwa Wazazi kuhusu Usalama na Ufikiaji wa maelezo nyeti.....	12
Marekebisho ya Rekodi Mzazi Anapotuma Ombi.....	16
Kurejelea na Hatua ya mamlaka ya utekelezaji sheria na mamlaka za mahakama na Kuhamishwa kwa Rekodi	18
WAZAZI KUWAPELEKA WATOTO WAO KATIKA SHULE ZA KIBINAFSI	19
Wazazi Kuwapeleka Watoto wao katika Shule za Kibinafsi.....	19
Wazazi Kuwapeleka Watoto Wao kwenye Shule za Kibinafsi ikiwa wana tatizo la FAPE.....	19
NIDHAMU KWA WATOTO WENYE ULEMAVU	21
Nidhamu Kwa Watoto Wenye Ulemavu.....	21
Mabadiliko ya Usajili kutokana na Utovu wa Nidhamu	22
Dhihirisho Uamuzi na Matokeo Yanayotarajiwa	23
Hali Maalum na Matokeo yanayotarajiwa.....	24
Mchakato yakinifu wa Kusikiliza malalamishi kuhusu Kuwaadhibu Wanafunzi wenye Ulemavu	24
Ulinzi wa Watoto Wasiobainishwa Kustahiki kwa Elimu ya Walio na Ulemavu na Huduma Husika	26
UTARATIBU WA KUTATUA MZOZO KATIKA JIMBO	27
Malalamishi ya Jimbo	27
Upatanisho.....	29
Mchakato Yakinifu wa Kusikizwa kwa Malalamishi.....	31
Kusikizwa Bila Kubaguliwa Mahakamani	31
Haki za Kusikizwa	32

Ufichuzi Zaidi wa Maelezo	32
Haki za Wazazi katika Kusikizwa kwa Kesi	33
Maamuzi ya Kusikizwa	33
Afisa Anayesikiliza Kesi Bila Ubaguzi	33
Vipindi vya Kusikizwa	34
Hali ya Mtoto Wakati wa Kusikizwa kwa Kesi (“Usihofu”)	34
Utoshelevu wa Malalamishi	35
Jibu la Wilaya kwa Ombi la Mchakato wa Kusikizwa kwa Malalamishi Lililotumwa na Mzazi	35
Jibu la Mhusika Mwingine kwa Mchakato Yakinifu wa Kusikizwa kwa Malalamishi.....	36
Mkutano wa Uamuzi	36
Kipindi cha Siku 30 za Kutafuta Suluhu	36
Mabadiliko kwenye Kipindi cha Uamuzi cha siku 30	37
Mkataba wa Kufidia Ulioandikwa	37
Jambo Muhimu katika Mchakato yakinifu wa Kusikizwa kwa Kesi	37
Uamuzi wa Mwisho.....	38
Hatua za Kiraia	38
Ada ya Wakili	38
Matokeo na Uamuzi kwa Bodi ya Ushauri na Raia kwa Ujumla	39
UHAMISHAJI WA HAKI	40
Uhamishaji wa Haki za Wazazi katika Umri wa Wengi	40
UFUPISHO NA UFAFANUZI	41
REJELEO.....	41

Haki ulizo nazo, kama mzazi wa mtoto aliye na ulemavu, zimefafanuliwa kwenye hati hii na pia zinapatikana katika Elimu ya Walemavu katika jimbo la South Dakota ***Masharti ya Usimamizi wa South Dakota (ARSD)***, [Article 24:05](#). Marejeleo mahususi katika Sheria za Usimamizi yameorodheshwa inavyofaa. Kwa kuwa ulinzi huu wa utaratibu unahitajika kwa mujibu wa IDEA, marejeleo mahususi ya kisheria kwa [Sehemu ya B ya IDEA \(34 CFR Part 300\)](#) yamebainishwa katika kila sehemu ya hati hii kama kipengee cha ziada cha kurejelea.

Hii imekusudia kutoa muhtasari wa taratibu za elimu kwa watu wenye ulemavu katika sheria ya South Dakota na ***Sehemu ya B*** ya IDEA (34 **CFR** Sehemu ya 300), sheria ya shirikisho. Tafadhali angalia masharti ya kisheria na kanuni ili upate lugha halisi inayotumika.

MAELEZO YA KIJUMLA

Upatikanaji wa Notisi ya Ulinzi wa Utaratibu

34 CFR 300.504(a) na (b); ARSD 24:05:30:06.01

Sharti upewe nakala ya notisi ya ulinzi wa utaratibu, mzazi wa mtoto aliye na ulemavu, angalau mara moja kila mwaka wa shule. Sharti upewe pia nakala:

1. Baada ya rejeleo au ombi lako la awali la kutathmini mtoto wako;
2. Unapotuma ombi;
3. Mtoto wako anapoadhibiwa kwa namna ambayo inabadilisha usajili wake;
4. Baada ya kuripoti malalamishi yako ya kwanza kwa shirika la Kitaifa au **Mchakato Yakinifu** wa kusikiliza malalamishi katika mwaka wa shule.

Nakala ya notisi ya ulinzi wa utaratibui inaweza pia kuchapishwa kwenye tovuti ya utawala wa shule.

Idhini ya Mzazi

34 CFR 300.9; ARSD 24:05:25:02.01, 24:05:25:02.02

"**Idhini**" inamaanisha kuwa umepokea maelezo yote yanayohitajika ili uweze kuelewa shughuli inayofafanuliwa na unakubali kuikamilisha kwa kuandika. Kwa namna hii, unaweza kutoa idhini yako. Sharti utoe maelezo haya katika lugha au njia yako ya asili ya mawasiliano. Ikiwa shughuli ambayo unaombwa kutoa idhini inahusu kutuma rekodi za mtoto wako, utarifiwa kuhusu rekodi ambazo utatuma na yule ambaye unaweza

Lugha ya Asili

34 CFR 300.29

(a) Lugha ya Asili, inapotumiwa na mtu asiye na umilisi wa Kiingereza, inamaanisha:

Lugha ambayo mtu huyu hutumua,

kumtumia rekodi hizi. Una hiari ya kutoa idhini na unaweza kuibatilisha wakati wowote.

Ubatilishaji wa idhini utatumika tu kwa shughuli za baadaye wala sio kwa zile ambazo tayari zimetendeka. Ukibatilisha idhini ya mtoto wako kupokea elimu kwa walemavu kwa kuandika na **huduma husika** baada ya mtoto wako kuanza kupokea elimu na huduma hizi, utawala wa shule hauhitajiki kuondoa maelezo yoyote kutoka kwenye rekodi za kimasomo ya mtoto wako kuhusu elimu maalum na huduma kama hizi ambazo alipokea kabla uondoe idhini yako. Baada ya kuupa utawala wa shule ubatilishaji kwa kuandika (kughairi) idhini yako, wilaya ya shule sharti ikupe ilani ya mapema kwa kuandika kisha iache kumpa mtoto wako elimu kwa walemavu na huduma kama hizi.

Idhini ya Tathmini ya Awali

34 CFR 300.300(a); 34 CFR 300.45; ARSD 24:05:25:02.01; ARSD 24:05:15:06

Utawala wa shule yako sharti utoe ilani kwa kuandika na kupata idhini yako kabla ya kuanza tathmini ya awali kwa mtoto wako ili kubaini ikiwa anastahiki kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA kupokea elimu kwa watu walio na ulemavu na huduma kama hizi.

1. Utawala wa shule yako sharti ujitahidi kupata idhini kabla ya kumtathmini mtoto wako.
2. Idhini yako ya tathmini ya kwanza haimaanishi kuwa umekubali mtoto wako apatiwe elimu maalum na huduma kama hizi.
3. Ikiwa mtoto wako amejiunga au anajaribu kujiunga na shule ya umma na ukatae afanyiwe tathmini kwa mara ya kwanza au ukose kujibu ombi la kuidhinisha ili afanyiwe tathmini hii, utawala wa shule unaweza, ingawa si lazima, kutumia utaratibu wa utatuzi wa mzozo wa IDEA (yaani, upatanisho, mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi) kushughulikia kutotoa kwako kwa idhini ya kumtathmini mtoto wako.
4. Ikiwa utawala wa shule yake hautumi ombi la tathmini kupitia utaratibu wa kutatua mizozo kupitia IDEA (yaani, upatanisho, kuhusu mchakato yakinifu wa kusikiliza

au, akiwa ni mtoto, lugha ambayo wazazi wake hutumia, isipokuwa inavyobainishwa katika aya ya (a)(2) ya sehemu hii.

Katika mwingiliano wowote wa moja kwa moja na mtoto (ikijumuisha kumtathmini mtoto), lugha ambayo mtoto hutumia nyumbani au shuleni.

(b) Kwa mtu aliye na ulemavu wa kusikia au kuona, au asiye na uwezo wa kuandika, msimbo wa mawasiliano ni ule ambao huwa anatomia (kama vile lugha ya ishara, Maandishi ya Vipofu au mazungumzo)

Ufafanuzi wa Mzazi

34 CFR 300.30; ARSD 24:05:13:04

1. Mzazi asili au mlezi wa mtoto;
2. Mzazi wa kambo isipokuwa anapokatazwa na sheria, masharti au mkataba;
3. Mlezi aliyeteuliwa na mahakama na kuidhinishwa kuwa kama mzazi wa mtoto, au kufanya uamuzi wa kielimu kwa niaba ya mtoto;
4. Mtu anayechukua nafasi ya mzazi pasipo mzazi mlezi au wa kiasili (akijumuisha babu na nyanya, mzazi wa kambo, au jamaa mwingine) ambaye mtoto anaishi naye, au mtu aliyeidhinishwa kisheria kuwajibikia maslahi ya mtoto;
5. Mzazi mlezi anayeteuliwa kwa mujibu wa kanuni za elimu kwa walemavu; **au**
6. Mtu au watu fulani ambao Mahakama inaamuru kuwa kama "mzazi" wa mtoto au kufanya maamuzi ya kielimu kwa niaba ya mtoto.

malalamishi), hautakuwa umekiuka haki za mtoto katika wajibu wa kupata, kubaini na kutathmini mtoto wako au masharti yanayohusu idhini ya mzazi, tathmini na kutathmini upya.

Ikiwa mtoto anachuliwa kuwa na mlezi kwa mujibu wa sheria ya Jimbo na haishi na mzazi wake, utawala wa shule hauhitaji idhini ya mzazi ili kumtathmini kubaini ikiwa ana ulemavu ikiwa:

1. Utawala wa shule umeshindwa kumpata mzazi baada ya juhudi za kumtafuta;
2. Haki za mzazi zimebatilishwa kwa mujibu wa sheria ya Jimbo; **au**
3. Hakimu amemkabidhi mtu ambaye si mzazi wa mtoto, haki ya kufanya uamuzi wa kielimu ikijumuisha tathmini ya kwanza, na mtu huyu ametoa idhini yake.

Idhini ya Huduma

34 CFR 300.300(b)

Utawala wa shule yako sharti upate idhini kabla ya kumpa mtoto wako elimu kwa walemavu kwa mara ya kwanza.

1. Utawala wa shule sharti upate idhini kabla ya kumpa mtoto wako elimu kwa watu wenye ulemavu na huduma kama hizi **kwa mara ya kwanza**.
2. Ikiwa hujibu ombi la kuidhinisha mtoto wako ili kupokea elimu kwa watu wenye ulemavu na huduma kama hizi kwa mara ya kwanza, au ukikataa kutoa idhini hii, au kubatilisha idhini yako baadaye kwa kuandika, utawala wa shule yako **huenda usitumie** utaratibu wa utatuzi wa mzozo wa IDEA (yaani, upatanisho, mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi) ili kufanya uamuzi kuondoa idhini ya mtoto wako ili kupokea elimu hii na huduma kama hizi.
3. Ikiwa hujibu ombi la kuidhinisha mtoto wako ili kupokea elimu kwa walemavu na huduma kama hizi kwa mara ya kwanza, au ukikataa kutoa idhini yako, au kubatilisha idhini yako baadaye kwa kuandika, utawala wa shule yako **huenda usitumie** utaratibu wa utatuzi wa mzozo wa IDEA

Ikiwa wewe ni mlezi au mzazi wa kiasili wa mtoto, unachukuliwa kuwa mzazi isipokuwa ikiwa huna mamlaka ya kisheria kufanya maamuzi ya kimasomo kwa niaba ya mtoto wako.

Jimbo haliwezi kuwa mzazi ikiwa mtoto ana mlezi.

Ufafanuzi wa Mtoto kuwa na Mlezi

34 CFR 300.45; ARSD 24:05:13:01

Mtoto kuwa na Mlezi, kama inavyotumika katika IDEA, inamaanisha mtoto ambaye:

1. Mtoto wa kambo;
2. Anachukuliwa kuwa na Mlezi kwa mujibu wa sheria ya Jimbo; au
3. Anatumizwa na shirika la umma la kutunza maslahi ya watoto.

Isipokuwa:

Sheria kwa mtoto aliye na mlezi haijumuishi mtoto wa kambo aliye na mzazi wa kambo anayetimiza masharti ya kuitwa mzazi.

Ufafanuzi wa Mzazi Mlezi

34 CFR 300.519; ARSD 24:05:30:15

Kila utawala wa shule utabaini utaratibu wa kukabidhi mzazi mlezi ili kuhakikisha kuwa haki za mtoto zimelindwa ikiwa hakuna mzazi, kama inavyobainishwa katika § 24:05:13:04, anayetambulika na wilaya baada ya kuweka juhudi, imeshindwa kumpata mzazi au ikiwa mtoto anachukuliwa kuwa na mlezi kwa mujibu wa sheria ya jimbo au ikiwa ni mwanarika asiye na kwao anayejiwasilisha kama inavyobainishwa katika kifungu cha 725(6) ya Sheria ya McKinney-Vento Homeless Assistance,

(yaani, upatanisho, kutoa malalamishi ya kusikizwa mahakamani) ili kufanya uamuzi wa kuondoa idhini ya mtoto wako katika kupokea elimu maalum na huduma kama hizi, utawala wa shule:

- a. Haujakiuka masharti ya kumpa mtoto wako **elimu inayofaa ya umma isiyo ya malipo (FAPE)** kwa kukosa kumpa huduma hizo; **na**
- b. Haupaswi kuwa na mkutano wa **mpango maalum wa elimu (IEP)** au kubuni IEP kwa mtoto wako ili kubaini elimu maalum na huduma kama hizi.

(1) Utambuzi wa wafanyakazi katika wilaya au kwenye jengo ambao wanahusika katika kuwapendekeza wanafunzi wanaohitaji mzazi mlezi;

(2) Utoaji wa mafunzo ya ndani kwa kigezo katika kipengele hiki cha kubaini ikiwa mtoto anahitaji mzazi mlezi; na

(3) Kubuni mfumo wa upendekezaji katika wilaya ya kuteua mzazi mlezi.

Ukibatilisha idhini yako kwa kuandika baada ya mtoto wako kupata elimu kwa watu wenye ulemavu na huduma kama hizi, basi utawala wa shule sharti ukuandikie kukupa ilani ya mapema, kama inavyofafanuliwa kwenye mada **Ilani ya Kuandikwa Mapema** na sharti iache kumpa mtoto wako huduma hizi baada ya kukupa ilani.

Idhini ya Kutathmini Upya

34 CFR 300.300(c) na (d); ARSD 24:05:25:06.01

Utawala wa shule sharti ukuombe idhini kabla ya kumtathmini mtoto wako upya, isipokuwa wilaya hii inaweza kudhihirisha na kuonesha hati kuwa:

1. Imefuata hatua zinazohitajika kupata idhini ya kumtathmini mtoto wako upya; **na**
2. Hukujibu.

Katika tathmini za awali, utawala wa shule haukiuki matokeo ya mtoto na majukumu mengine kwenye Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa haifuatili utathmini upya usipopeana idhini.

Utawala wa shule sharti udumishe rekodi za juhudi za kupata idhini yako kwa tathmini za awali, kutoa elimu kwa walemavu na huduma kama hizi kwa mara ya kwanza, kutathmini upya na kutatufa wazazi wa watoto ambao wanachukuliwa kuwa walezi na kufanyiwa tathmini ya kwanza. Hati hii sharti iwe na rekodi ya majaribio ya utawala wa shule katika sehemu zifuatazo:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au zilizojaribiwa kupigwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za mawasiliano ulizotumiwa na majibu yoyote uliyopokea; **na**
3. Rekodi ya kina ya ziara zilizofanywa nyumbani kwako au mahali pa kazi na matokeo ya ziara hizi.

Masharti mengine ya idhini

34 CFR 300.300(d); ARSD 24:05:25:02.03

Utawala wa shule **hauhitaji** idhini yako kabla ya:

1. Kukagua data iliyopo kama sehemu ya kumtathmini mtoto wako kwa mara ya kwanza na upya;
2. Kumpa mtoto wako jaribio au tathmini nyingine inayopewa watoto wengine isipokuwa, kabla ya kumpa jaribio hilo, idhini kutoka kwa wazazi wote inahitajika.

Utawala wa shule unaweza kutumia kutotoa idhini kwako kwa utathmini au kupata huduma katika IDEA kutokukuruhusu au mtoto wako kupata huduma nyingine, manufaa au shughuli, isipokuwa inavyohitajika katika Sehemu ya B ya IDEA.

kiwa umemwandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa gharama yako mwenyewe au ikiwa unamsomesha nyumbani, na hujatoa idhini ya tathmini ya kwanza au kumtathmini upya, au umekosa kujibu ombi la kutoa idhini, utawala wa shule hauwezi kutumia utaratibu wa kutatua mizozo wa IDEA (yaani, upatanisho, mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi) kubatilisha uamuzi wako. Katika hali kama hizi, utawala wa shule hauhitajiki kumchukulia mtoto wako kama anayestahiki kupokea huduma sawa (hudumu wanazopokea watoto walio na ulemavu waliowekwa na wazazi katika shule za kibinafsi, kwa mujibu wa sheria ya SD na watoto wanaosomeshwa nyumbani hawastahiki kupokea huduma sawa).

Ilani ya Kuandikwa Mapema

34 CFR 300.503; 34 CFR 300.505; 34 CFR 300.304; ARSD 24:05:30:04

Utawala wa shule sharti ukupe **Ilani ya Kuandikwa Mapema** angalau **siku** tano za kazi kabla ya kupendekeza au kukataa kuanza au kubadilisha utambulisho, tathmini, usajili wa kielimu au kumpa mtoto wako FAPE. Unaweza kutupilia mbali ilani iliyoandikwa ikiwa ungependa mabadiliko haya yaanze kabla ya siku tano zinazohitajika kupata ilani.

Ilani ya kuandikwa mapema sharti:

1. Ifafanue hatua ambayo utawala wa shule unapanga au unakataa kuchukua;
2. Ieleze sababu ya utawala wa shule kupanga au kukataa kuchukua hatua hii;
3. Ifafanue kila utaratibu wa tathmini, ukadiriaji, rekodi au ripoti ambayo utawala wa shule umetumia katika kuamua kupanga au kukataa kuchukua hatua;
4. Ijumuishe taarifa kwamba unalindwa kwa mujibu wa sheria za utaratibu wa ulinzi katika Sehemu ya B ya IDEA;

5. Ikujulishe mahali ambapo unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu ulinzi wa utaratibu ikiwa hatua inayopangiwa au kukataliwa si pendekezo la awali la tathmini;
6. Ijumuishe anwani ya mawasiliano ya nyenzo za kukusaidia kuelewa Sehemu ya B ya IDEA;
7. Ifafanue chaguo zingine ambazo **Timu ya IEP** ya mtoto wako ilikubali na sababu za kukataliwa kwa chaguo hizi;
8. Ifafanue mambo mengine ambayo utawala wa shule ulitumia katika uamuzi wake wa kupangia au kukataa hatua; **na**
9. Ikiwa utawala wa shule yako unapanga kufanya utathmini, fafannua utaratibu wowote ambao unapanga kufuata.

Ilani ya kuandikwa mapema sharti:

1. Iandikwe katika lugha inayoeleweka kwa urahisi; **na**
2. Iandikwe katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano, isipokuwa isiwezekane kufanya hivyo.

Ikiwa lugha yako au njia nyingine ya mawasiliano si ya kuandikwa, utawala wa shule sharti uchukue hatua kuhakikisha kwamba:

1. Umetafsiriwa ilani hii kwa njia ya mdomo katika mbinu nyingine kwenye lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano;
2. Unaelewa maudhui kwenye ilani;na
3. Kuna hati inayoonesha kuwa umetimiza masharti ya 1 na 2.

Unaweza kuchagua kupokea ilani za kuandikwa mapema, hati za utaratibu wa ulinzi wa haki za wazazi na zinazohusiana na upatanisho, mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi kupitia barua pepe, panapohitajika. Utawala wa shule utathibitisha kuwa ungependa kupokea ilani kupitia barua pepe.

Tathmini Huru ya Elimu (IEE)

34 CFR 300.502; ARSD 24:05:30:03

Una haki ya kupata *IEE* ya mtoto wako kwa gharamiwa ya umma, ikiwa haukubaliani na tathmini ya utawala wa shule.

IEE ni utathmini unaofanywa na mtahini aliyefuzu ambaye hajaajiriwa na utawala wa shule.

Gharama ya umma inamaanisha kuwa utawala wa shule unalipa gharama yote ya tathmini au unahakikisha kuwa tathmini inafanywa bila kukugharimu chochote kwa kuzingatia Sehemu ya B ya IDEA.

Ukituma ombi la IEE, utawala wa shule unaweza kukuuliza sababu yako ya kupinga tathmini ya shule. Una haki ya kutoeleza sababu yako ya kupinga.

Unapotuma ombi la IEE, wilaya ya shule itakupa maelezo kuhusu unapoweza kuipata na vigezo vinayotumika katika utawala wa shule kufanya IEE.

Ikiwa unahitajika kufanya IEE kwa gharama ya umma, kigezo cha tathmini ya utawala wa shule, ikijumuisha eneo la tathmini na kustahiki kwa mtahini, sharti iwe sawa na kigezo ambacho utawala huu unatumia wakati wa kutekeleza tathmini yake. Isipokuwa kupitia vigezo vilivyofafanuliwa hapo juu, utawala wa shule hauwezi kuweka masharti ya ziada au muda wa kupata IEE.

Sharti utawala wa shule upeane IEE kwa gharama ya umma, ama upige ripoti ya mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi kuonyesha kuwa tathmini ya utawala wa shule ilistahili kufanywa au kuwa IEE unayoomba au uliyo nayo inakiuka vigezo vya utawala wa shule.

Utawala wa shule ukipiga ripoti ya mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi ya kuomba kusikizwa na uamuzi wa hakimumu wa kushughulikia masuala ya mizozo ni kuwa tathmini ya utawala wa shule inafaa, bado una haki ya kupata IEE, lakini si kwa gharama ya utawala wa shule.

Unaweza tu kupata IEE moja ya mtoto wako kwa gharama ya umma kila utawala wa shule unapomtathmini mtoto wako.

Ukipata IEE kwa gharama ya shule au kutumia utawala wa shule tathmini iliyofanya kwa gharama ya kibinafsi, Timu ya IEP **sharti ikubali** IEE yoyote au tathmini zingine unazotuma ambazo zinazingatia vigezo vya wilaya ya shule ya IEES katika uamuzi wowote unaofanywa kuhusu kumpa mtoto wako FAPE.

Matokeo ya IEE yanaweza kuwasilishwa na upande wowote kama ushahidi katika mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa kesi inayohusu mtoto wako.

Ikiwa hakimumu wa kushughulikia mizozo ataomba IEE kama mojawapo wa ushahidi katika mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi, gharama ya tathmini sharti ilipwe na utawala wa shule.

Usalama wa maelezo na ufikiaji wa rekodi za elimu

34 CFR 300.611-617; ARSD 24:05:29; 34 CFR 300.622-625; 34 CFR 300.32

Sheria ya Elimu ya Familia na Ufaragha (FERPA) inawapa wazazi na wanafunzi walio na miaka 18 au zaidi (“wanafunzi wanaostahiki”) haki fulani kulingana na rekodi za mwanafunzi ikijumuisha haki ya ufikiaji (kukagua) rekodi na kisha kulinda usalama wa rekodi hizi. IDEA inaangazia pia ufikiaji na usalama wa rekodi.

Ilani kwa Wazazi kuhusu Usalama na Ufikiaji wa maelezo nyeti

Kwa mujibu wa FERPA, shule sharti iwaarifu wazazi wanaohudhuria kuhusu haki zao katika FERPA. Arifa ya kila mwaka sharti ijumuishe maelezo yanayohusu haki ya mzazi katika kukagua rekodi za elimu za mtoto wake, haki ya kuomba kurekebishwa kwa rekodi hizi, haki ya kuidhinisha ufichuzi wa **maelezo ya kutambulisha mtu binafsi (PII)** kwenye rekodi (isipokuwa katika hali maalum) na haki ya kutoa malalamishi katika Afisi ya Kufuata Sera ya Familia katika Idara ya Elimu Marekani kuhusu tuhuma za shule katika kufuata FERPA. Shule sharti pia iwaeleze wazazi fafanuzi za dhana "mfanyakazi wa shule" na "maslahi halali ya elimu."

Kwa mujibu wa FERPA shule haihitajiki kuwaarifu wazazi kuhusu haki zao mmoja baada ya mwingine. Badala yake, shule inaweza kupeana arifa ya kila mwaka kwa njia yoyote ambayo inaweza kuwaarifu wazazi kuhusu haki zao.

Kwa mujibu wa FERPA na IDEA, utawala wa shule:

Sharti ukuruhusu kukagua na kupekua rekodi zozote za elimu za mtoto wako ambazo hukusanywa, kuhifadhiwa na kutumiwa na utawala wa shule kwa mujibu wa sehemu ya B ya IDEA;

1. Sharti ukubali ombi lako la kukagua na kupekua rekodi za mtoto wako bila kucheleweshwa na kabla ya mkutano wowote wa IEP, kipindi cha utatuzi au mchakato yakinifu wa

Rekodi za Elimu

34 CFR 300.611(b), 34 CFR Part 99.;
Authority: 20 U.S.C. 1232g(a)(4))

FERPA

Kanuni ya Elimu ya Familia na Ufaragha (FERPA) ni sheria ya jimbo inayowapa wazazi haki ya kufikia rekodi za elimu za watoto wao, haki ya kuomba rekodi hizi zirekebishwe na haki ya kudhibiti ufichuzi wa maelezo ya utambulisho wa kibinafsi kwenye rekodi za elimu. Mtoto anapofikisha umri wa miaka 18, au anapojiunga na taasisi baada ya sekondari akiwa na umwri wowote, haki katika FERPA huamishwa kutoka kwa mzazi hadi kwa mwanafunzi (“mwanafunzi anayestahiki”).

(a) Dhana hii inamaanisha rekodi ambazo:

1. Zinazomhusu mwanafunzi kwa njia ya moja kwa moja; **na**
2. Inadumishwa na shirika la kielimu au taasisi au mtu mwingine anayewakilisha shirika au taasisi.

(b) Dhana hii haijumuishi:

1. Rekodi za wataalamu wa kufunza, wasimamizi na wakurugenzi na wataalamu wa elimu wanaowasaidia watu wanaomiliki rekodi na haiwezi kufikiwa au kufichuliwa kwa mtu mwingine yeyote isipokuwa msaidizi wa muda wa mtengeneza rekodi;
2. Rekodi za kiengo cha mamlaka ya kisheria ya shirika au taasisi ya elimu, lakini ikiwa tu rekodi zinazohifadhiwa na shirika au

kusikiliza kesi (inahusu utambuzi, tathmini, usajili wa kielimu, nidhamu au masharti ya FAPE); **na**

2. Haitachukua zaidi ya siku 45 za kazi kukubali baada ya ombi kutumwa.

Haki yako ya kukagua na kupekua rekodi za elimu inajumuisha:

1. Haki ya kupata jibu kutoka kwa utawala wa shule kwa maombi yanayofaa ya ufafanuzi na ufasiri wa rekodi.
2. Haki ya kuomba utawala wa shule ukupe nakala ya rekodi zilizo na maelezo ikiwa kukosa kupewa nakala hizi kutakuzuia kutumia haki yako ya kukagua na kupekua rekodi; **na**
3. Haki ya kuwa na uwasilishaji wa ukaguzi wako.

Utawala wa shule unaweza kuchukulia kuwa wewe una mamlaka ya kukagua rekodi za mtoto wako isipokuwa unapoarifiwa kuwa huna mamlaka haya.

Utawala wa shule sharti uhifadhi rekodi ya watu wanaopata idhini ya kufikia rekodi za elimu zinazokusanywa, kuhifadhiwa na kutumiwa katika Sehemu ya B ya IDEA (isipokuwa wewe au wafanyakazi wa wilaya ya shule wanaokubaliwa kufikia) ikijumuisha jina la mtu, tarehe alipokubaliwa kufikia na sababu anayoidhinishwa kutumia rekodi. Wewe au mwanafunzi anayestahiki mnaweza kuomba kukagua rekodi ya ufikiaji.

Ikiwa rekodi zozote za elimu zinajumuisha maelezo ya zaidi ya mtoto mmoja, kila mzazi ana haki ya kukagua na kupekua tu maelezo ya mtoto wake au kuarifiwa kuhusu maelezo mahususi ya mtoto wake.

Utawala wa shule sharti ukupe, unapoomba, orodha ya aina ya rekodi za elimu na maeneo ambayo rekodi hizo zimekusanywa, kuhifadhiwa au kutumiwa na wilaya ya shule.

Utawala wa shule unaweza kukutoza ada ya nakala za rekodi unazokabidhiwa kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa ada hii haikuzuilii kukagua rekodi hizi inavyofaa. Utawala wa shule huenda usikutoze ada kwa kutafuta au kupata maelezo kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

taasisi hazijafichuliwa kwa kitengo na trekodi za mamlaka ya sheria zimehifadhiwa tofauti na rekodi za elimu, zimehifadhiwa tu kwa madhumuni ya kutekeleza sheria na kufichuliwa tu kwa maofisa walinda usalama wa wilaya hii;

3. Rekodi za mtu aliyeajiriwa kwenye shirika au taasisi ya elimu zinazobuniwa na kuhifadhiwa kutokana na shughuli za kawaida, zinazomhusu tu mtu huyu katika hadhi yake kama mfanyakazi na haziwekwi ili kutumika kwa madhumuni mengine yoyote. Rekodi za mtu anayejiwasilisha katika shirika au taasisi ambaye anaajiriwa kulingana na hadhi yake kama mwanafunzi ni za kielimu na hazihitajiki katika sehemu hii;
4. Rekodi za mwanafunzi aliye na umri wa miaka 18 au zaidi, au anayehudhuria taasisi ya masomo baada ya sekondari, ambazo:

(i) Zimeandikwa na kuhifadhiwa na daktari, daktari wa kutibu akili, mwanasaikolojia, au wataalamu wengine maarufu wanaofanya kazi yao au kusaidia katika kufanya kazi hii;

(ii) Zilizobuniwa, kuhifadhiwa au kutumiwa katika kutibu mwanafunzi; na

(iii) Zinafichuliwa tu kwa watu wanaotoa huduma za matibabu. Kwa madhumuni ya ufafanuzi

Sharti utoe idhini kabla ya maelezo ya kukutambulisha yatumwe kwa watu wengine, isipokuwa inaporuhusiwa na FERPA au IDEA.

Kwa mujibu wa IDEA, hauhitajiki kupeana idhini kabla ya maelezo ya kukutambulisha yatumwe kwa maafisa wa mashirika yanayoshiriki katika kukusanya au kutumia maelezo hayo katika Sehemu ya B ya IDEA, isipokuwa kwamba:

1. Sharti wewe au mwanafunzi anayestahiki apeane idhini kabla ya maelezo yanayokutambulisha yatumwe kwa maafisa ya mashirika husika yanayotoa au kulipia **huduma za mabadiliko**; na
2. Ikiwa mtoto wako yuko, au atajiunga na shule ya kibinafsi, sharti upeane idhini kabla ya maelezo yoyote ya kukutambulisha yatumwe kwa maafisa katika utawala wa shule ya umma ya mtoto wako ambapo shule ya kibinafsi inapatikana na maafisa wa utawala wa shule ambapo mtoto wako anaishi.

Kwa mujibu wa FERPA, hauhitajiki kupeana idhini kabla ya maelezo ya kukutambulisha yatumwe:

1. Kwa maafisa wengine wa shule, wakiwemo walimu, katika utawala wa shule yako ambao shule imebaini kuwa wana haki ya kisheria kufaidika na elimu. Wanajumuisha wanakandarasi, washauri, wafanyakazi wa kujitolea au watu wengine ambao shule imewaomba kutoa huduma au kutekeleza majukumu ya taasisi, ikiwa wametimiza masharti.
2. Kwa maafisa wa shule nyingine, mfumo wa shule au taasisi ya masomo baada ya sekondari ambapo mtoto wako anataka au angependa kujiunga, au mahali ambapo mtoto wako tayari amesajiliwa ikiwa ufichuzi huu ni kwa madhumuni yanayohusiana na kijiunga au kuhamisha mtoto wako, ikiwa ametimiza masharti (haswa, ikiwa ilani ya kila mwaka inamwarifu mzazi kuwa shule huonesha rekodi isipokuwa kwa sababu hii, au shule inajaribu kadri iwezavyo kukuarifu au mwanafunzi anayestahiki katika anwani ulioandika hapo awali, au ufichuzi huu umefanywa na wewe au mwanafunzi).
3. Kuidhinisha wawakilishi wa Mhasibu Mkuu wa Marekani, Mwanasheria Mkuu wa Marekani, Katibu wa Elimu Marekani, au mamlaka ya elimu katika Jimbo au manispaa, kama vile Idara ya Elimu ya South Dakota. Ufichuzi katika sheria hii unaweza kufanywa, kwa mujibu wa masharti yanayotumika, unaohusiana na uhasibu au tathmini ya mipango ya elimu inayofadhiliwa na Nchi au Jimbo, au kwa kutekeleza au kuzingatia masharti ya kisheria ya Jimbo yanayohusu mipango hiyo. Mashirika haya yanaweza kufichua zaidi maelezo ya kukutambulisha kwa mashirika mengine ambayo wamebainisha kuwa wawakilishi wao walioidhinishwa kufanya ukaguzi, tathmini au kutekeleza au kuangalia ikiwa yamezingatia masharti.

huu, "matibabu" hayajumuishi shughuli za ziada au ambazo haziko kwenye mpango wa kufunza katika shirika au taasisi;

5. Rekodi zilizobuniwa au kupokewa na shirika au taasisi ya elimu baada ya mtu kuacha kuwa mwanafunzi na zisizohusu mwanafunzi kuhudhuria kwa njia ya moja kwa moja; na
6. Alama za karatasi za kundi la

4. Kutokana na msaada wa kifedha ambao mtoto wako ametuma ombi au amepokea, ikiwa maelezo yanahitajika kwa madhumuni haya kama vile kubaini ustahiki wa kupata msaada, kiasi cha msaada, masharti ya msaada au kutekeleza vigezo na masharti ya msaada.
5. Kwa maafisa wa Nchi au manispaa au mamlaka ambayo yanaruhusiwa kupokea au kufichuliwa maelezo haya kwa mujibu wa Sheria ya Nchi inayohusu mfumo wa haki ya watoto na uwezo wa mfumo huu kutoa huduma kwa urahisi, kabla ya uamuzi, mwanafunzi ambaye rekodi zake zilitolewa, kwa mujibu wa masharti husika.
6. Kwa mashirika yanayofanya utafiti kwa, au, kwa niaba ya, shule, ili: (a) kubuni, kuhalalisha, au kupeana majaribio ya kubaini;(b) kupeana mipango ya kusaidia mwanafunzi; au (c) kuboresha mbinu za kufunza, ikiwa zimetimiza masharti husika.
7. Kwa mashirika yanayopeana vyeti ili kutekeleza majukumu yake ya kutoa vyeti hivi.
8. Kwa mtoto wako ikiwa ni mwanafunzi anayestahiki, mradi mwanafunzi huyu anakutegemea kwa madhumuni ya kodi ya IRS.
9. Kuzingatia amri ya mahakama au ilani iliyotolewa kisheria, ikiwa masharti husika yametimizwa.
10. Kwa maafisa husika kutokana na dharura ya kiafya au usalama, kwa mujibu wa masharti.
11. Ambayo imebainishwa na shule kama “maelezo elekezi,” mradi itimize masharti.
12. Kwa mfanyakazi wa shirika anayeshughulikia kesi au mwakilishi mwingine wa Nchi au shirika la maslahi ya watoto katika eneo lako au shirika la kikabila linaloruhusiwa kufikia mpango wa kesi wa mwanafunzi wakati shirika hilo lina jukumu la kufanya hivyo kisheria, kwa mujibu wa sheria ya Nchi au kabila, kwa kumtunza na kumlinda mtoto anapokabidhiwa mzazi wa kambo.
13. Kwa Katibu wa Kilimo au wawakilishi wa Huduma ya Chakula na Lische kwa madhumuni ya kutekeleza ufuatiliaji, tathmini na kukadiria utendakazi wa mipango inayoidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni ya Richard B. Russell National School Lunch au Kanuni ya Child Nutrition Act ya 1966, katika hali fulani.

Shirika la elimu linalopokea maelezo ya kukutambulisha kutoka kwa shirika au taasisi nyingine inaweza kufanya ufichuzi zaidi wa maelezo haya kwa niaba ya shirika la elimu bila idhini yako au ya mwanafunzi anayestahiki ya kuandika mapema ikiwa imetimiza masharti ya IDEA au FERPA kuhusu ufichuzi bila idhini ya mzazi na shirika linapomwarifu mmiliki wa maelezo yanayofichuliwa kuhusu masharti haya.

Maelezo ya Utambulisho

Shule sharti ilinde usalama wa **PII katika** hatua za kukusanya, kuhifadhi, kufichua na kuharibu.

1. Afisa mmoja katika utawala wa shule sharti awajibike katika kuhakikisha usiri wa maelezo yoyote ya kukutambulisha.
2. Kila mtu anayekusanya au kutumia maelezo ya kumtambulisha mtu binafsi sharti apate mafunzo au kufunzwa kuhusu sera ya Jimbo na utaratibu kuhusu usalama wa maelezo haya kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na FERPA.
3. Wilaya sharti ihifadhi, kwa sababu ya ukaguzi wa umma, orodha ya sasa ya majina na vyeo vya wafanyakazi katika wilaya ambao wanaweza kufikia maelezo ya kibinafsi.
4. Wilaya sharti ikujulishe wakati ambapo maelezo yako ya kibinafsi yanayokusanywa, kuhifadhiwa au kutumiwa katika elimu ya walemavu au huduma husika hayahitajiki kwa minajili ya kumpa mtoto wako huduma za kielimu.
5. Maelezo yasiyohitajika tena sharti yafutwe unapotuma ombi;ingawa; rekodi ya kudumu ya jina la mtoto wako, anwani, namba ya simu, matokeo yake, rekodi ya kuhudhuria, vipindi alivyohudhuria na kiwango cha darasa alichokamilisha huenda yakahifahiwa kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa kanuni za Haki na Kanuni ya Elimu na Faragha ya Familia ya 1974 (34 CFR 99.5(a)), haki zako za rekodi za elimu hukabidhiwa mwanafunzi anapofikisha umri wa miaka 18. Kwa mujibu wa FERPA, mwanafunzi aliye na umri wa miaka 18 au zaidi anajulikana kama “mwanafunzi anayestahiki”.

Umri wa Wengi (mtoto anayefikisha umri wa miaka 18)

Wakati ambapo haki zako katika Sehemu ya B ya IDEA zinakabidhiwa mwanafunzi anayefikisha mwaka unaostahiki, sharti akabidhiwe pia haki za rekodi za elimu. Ingawa, utawala wa shule sharti ukupe wewe na mwanafunzi ilani yoyote inayohitajika kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA. (Angalia maelezo zaidi chini ya mada “Uhamishaji wa haki za Mzazi katika Umri Unaostahiki Kwenye ukurasa wa 38).

Marekebisho ya Rekodi Mzazi Anapotuma Ombi

34 CFR 300.618-621; ARSD 24:05:29:04

Ikiwa unaamini kuwa maelezo kwenye rekodi za elimu kuhusu mtoto wako si sahihi, yanapotosha au yanakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, unaweza kutuma ombi kwa utawala wa shule uyarekebishe au kuyaondoa (yaani, irekebishe rekodi).

Utawala wa shule sharti ufanye uamuzi ikiwa utarekebisha au kuondoa maelezo kwa muda unaofaa kutokana na ombi lako. Utawala wa shule ukiamua kukataa kurekebisha au kuondoa maelezo haya,

sharti ukujulishe na kukushauri kuhusu haki yako ya kusikizwa kwa mujibu wa Kanuni ya Elimu na Faragha ya Familia (**FERPA**)

Utawala wa shule sharti, unapotuma ombi, ukupe haki ya kusikizwa kwa mujibu wa FERPA ili uweze kupinga maelezo kwenye rekodi za elimu za mtoto wako ambayo unaamini si sahihi, yanapotosha au yanakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako.

Kesi ya kupinga maelezo kwenye rekodi za elimu sharti zisikizwe kwa kuzingatia utaratibu wa kesi hizo kwa mujibu wa FERPA.

Kanuni ya Haki ya Elimu na Faragha ya Familia (FERPA)

Kwa kawaida, utaratibu wa kusikizwa kwa kesi ya FERPA wa utawala wa shule sharti ukupe yafuatayo:

1. Kesi sharti isikizwe ndani ya siku 30 baada ya utawala wa shule kupokea ombi lako la kusikizwa na wewe au mwanafunzi anayestahiki sharti mpate ilani ya tarehe, mahali na wakati siku tano kabla ya kusikizwa;
2. Kesi hii inaweza kusikizwa na mtu yeyote, ikijumuisha afisa wa utawala wa shule, ambaye hatafaidika moja kwa moja kutokana na matokeo ya kesi hii;
3. Wewe au mwanafunzi anayestahiki sharti apewe fursa kamili na ya haki ya kuwasilisha ushahidi unaohitajika kwa kesi na mnaweza kusaidiwa au kuwakilishwa na watu unaowataka kwa gharama yako, ikijumuisha wakili;
4. Utawala wa shule sharti ufanye uamuzi wake kwa kuandika ndani ya siku 30 baada ya kesi kukamilika;na
5. Uamuzi wa utawala wa shule sharti utokane na ushahidi uliotolewa wakati wa kusikizwa kwa kesi na uwe na muhtasari wa ushahidi na sababu za kufikiwa kwa uamuzi huo.

Ikiwa, kutokana na kusikizwa kwa kesi, utawala wa shule utaamua kuwa maelezo haya ni sahihi na hayakiuki faragha ya mtoto wako, lakini hukubalini nayo, una haki ya kuandika taarifa. Hata hivyo, ikiwa kutokana na kusikizwa kwa kesi, utawala wa shule utaamua kuwa maelezo katika faili ya mtoto wako si sahihi sharti uondoe maelezo haya na kukuarifu kwa kuandika.

Uamuzi wowote unaowekwa kwenye rekodi za mtoto wako sharti yahifadhiwe na utawala wa shule kama sehemu ya rekodi za mtoto wako. Ikiwa rekodi hizi zenye utata za mtoto wako zimefichuliwa na utawala wa shule, sharti utawala huu ufichue uamuzi unaoafikiwa kwa watu wengine pia.

Kurejelea na Hatua ya mamlaka ya utekelezaji sheria na mamlaka za mahakama na Kuhamishwa kwa Rekodi

34 CFR 300.535(a) na (b); ARSD 24:05:26:15

Utawala wa shule unaweza kuripoti uhalifu ulioteklezwa na mtoto aliye na ulemavu kwa mamlaka yanayofaa. Hakuna kipengele kwenye IDEA kinachozuia mamlaka ya utekelezaji sheria katika Jimbo na mamlaka ya mahakama kutekeleza majukumu yao ya kutumia sheria ya Nchi na ya Jimbo kwa uhalifu unaotekelezwa na mtoto aliye na ulemavu.

Utawala wa shule unaporipoti uhalifu unaotekelezwa na mtoto aliye na ulemavu utawasilisha nakala za elimu kwa watoto walemavu na rekodi za nidhamu za mtoto ili ziweze kukaguliwa na mamlaka husika ambapo imeripoti uhalifu, lakini tu kwa kiwango kinachoruhusiwa na FERPA.

WAZAZI KUWAPELEKA WATOTO WAO KATIKA SHULE ZA KIBINAFSI

Wazazi Kuwapeleka Watoto wao katika Shule za Kibinafsi

34 CFR 300.504(a) na (b); ARSD 24:05:30:06.01

Ikiwa umemsajili mtoto wako katika shule au taasisi ya Kibinafsi na hujakiuka sheria ya FAPE, basi una hiari ya kufanya uamuzi wa kumsajili. Ikiwa utawala wa shule umempa mtoto wako FAPE katika shule, basi utawala huu haupaswi kulipia elimu kwa watu walio na ulemavu au gharama nyingine ya elimu ya kibinafsi ya mtoto wako. Hata hivyo, shule za umma hazina majukumu fulani kwa mujibu wa watoto wenye ulemavu waliopolekwa katika shule za kibinafsi kwa hiari wanaohudhuria shule za kibinafsi zinazopatikana katika mipaka yao ya kijiografia.

Ikiwa shule ya kibinafsi ya mtoto wako inatimiza masharti ya IDEA na ya shule za kibinafsi, shule ya umma ambapo shule ya kibinafsi inapatikana sharti:

1. Imuhesabu mtoto wako katika idadi yake ya watoto waliosajiliwa katika shule ya kibinafsi na wazazi wao.
2. Kumfanyia mtoto wako utathmini mpya wa mara kwa mara unaohitajika na IDEA, kwa mujibu wa idhini yako.
3. Kushauriana nawe na shule ya kibinafsi anapohudhuria mtoto wako kupata majibu kuhusu ugavi sawa wa fedha za IDEA Sehemu ya B zinapaswa kutumika katika elimu maalum na huduma husika kwa watoto wa shule za kibinafsi wanosajiliwa na wazazi wao ikijumuisha mtoto wako.
4. Baada ya kushauriana na maafisa wa shule ya kibinafsi na wawakilishi wa wazazi wa watoto waliosajiliwa na wazazi wao katika shule ya kibinafsi, kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu huduma zinazopaswa kutolewa kwa watoto walio na ulemavu wanaostahiki na waliosajiliwa katika shule ya kibinafsi na wazazi wao.

Uamuzi kuhusu aina na kiasi cha huduma ambazo watoto walio na ulemavu na waliosajiliwa na wazazi wao katika shule za kibinafsi watazipata, na hufanywa kutokana na kushauriana, na hutegemea mahitaji ya watoto wanaostahili kupokea huduma. Watoto waliosajiliwa katika shule za kibinafsi na wazazi wao hawana haki ya kibinafsi kupokea sehemu au elimu kamili na maalum na huduma husika ambazo wangepokea ikiwa wangesajiliwa katika shule ya umma.

Wazazi Kuwapeleka Watoto Wao kwenye Shule za Kibinafsi ikiwa wana tatizo la FAPE

34 CFR 300.148; ARSD 24:05:31:05

Kutoelewana kwako na utawala wa shule kuhusu upatikanaji wa mpango unaomfaa mtoto wako na suala la malipo ya kusajiliwa katika shule ya kibinafsi yanaweza kuamuliwa wakati wa mchakato yakinifu wa kusikiliza kesi. Afisa anayesikiliza kesi au mahakama inaweza kuhitaji utawala wa shule

anakoenda mtoto wako (unapoishi) kukurejeshea pesa ulizotumia katika shule ya kibinafsi, afisa au mahakama inapogundua kuwa shule ya umma haikumpa mtoto wako FAPE na kuwa ulilazimika kumsajili katika shule ya kibinafsi. Afisa anayesikiliza kesi au mahakama inaweza kuamua kuwa ulilazimika kumsajili, hata ikiwa usajili huu hautimizi vigezo vya Nchi vinavyotumika katika elimu inayotolewa na shule za umma.

Pesa unazofaa kurejeshewa huenda zikapunguzwa au kukataliwa na afisa anayesikiliza kesi au mahakama ikiwa:

1. Haukuiarifu, Timu ya IEP, katika mkutano wa mwisho uliohudhuria kabla ya kumsajili mtoto wako katika shule ya kibinafsi, kuwa haukukubaliana na usajili uliopendekezwa na utawala wa shule wa kumpa mtoto wako FAPE, ikijumuisha kutaja sababu zako na lengo la kumsajili mtoto wako katika shule ya kibinafsi badala ya shule ya umma, au badala yake, haukuipa wilaya ya shule ilani iliyoandikwa, angalau siku (10) za kazi (ikijumuisha likizo katika siku za kazi) kabla ya kumuondoa mtoto wako katika shule ya umma, ya kutokubaliana na usajili uliopendekezwa na utawala wa shule, ikijumuisha kutaja sababu na lengo lako la kumsajili mtoto wako katika shule ya kibinafsi badala ya ile ya umma; au
2. Kabla ya mtoto wako kuacha kuhudhuria shule ya umma, utawala wa shule ulikupa ilani ya kuandika mapema ya pendekezo lake la kutathmini mtoto wako, na ikajumuisha madhumuni ya kutathmini, lakini haukumpeleka mtoto wako kufanyiwa tathmini inayofaa na wilaya ya shule; na
3. Afisa anayesikiliza kesi au mahakama inapofanya uamuzi kuwa ulikiuka sheria.

Hata hivyo, pesa utakazorejeshewa hazitapunguzwa au kuondolewa kwa kukosa kuipa utawala wa shule ilani inayohitajika ya kutokukubali na lengo lako la kumsajili mtoto wako katika shule ya kibinafsi, ikiwa:

1. Shule ilikuzuia kuwasilisha ilani;
2. Hukupewa Utaratibu wa Ulinzi na Haki yako ya kuwa Mzazi ya South Dakota inavyohitajika, ya kukujulisha kuhusu jukumu lako la kutoa ilani kwa wilaya; au
3. Kufuata masharti haya ya kutohatarisha maisha ya mtoto wako.

Isitoshe, pesa utakazorudishiwa, kwa mujibu wa ushauri wa afisa anayesikiliza kesi na mahakama, hazitapunguzwa au kuondolewa kwa kutozingatia ilani za masharti, ikiwa:

1. Hujui kusoma au kuandika kwa lugha ya Kiingereza; **au**
2. Kufuata kwako kwa masharti ya ilani kutaathiri hisia za mtoto wako.

NIDHAMU KWA WATOTO WENYE ULEMAVU

Nidhamu Kwa Watoto Wenye Ulemavu

General Authority 34 CFR 300.530(a)-(d); ARSD 24:05:26:02.02; ARSD 24:05:26:02.01

Ikiwa mtoto wako aliye na ulemavu atakiuka maadili ya mwanafunzi, wahudumu wa shule wanaweza kumwondoa aliposajiliwa na kumpeleka katika **mazingira mbadala ya masomo kwa muda (IAES)** mazingira mengine, au kumfukuza mtoto wako, lakini **muda usizidi mfululizo wa siku 10 za shule**, kwa kiwango kinachoruhusiwa kwa watoto walio na ulemavu. Anaweza pia kuondolewa kwa siku 10 zaidi za shule katika mwaka mmoja wa shule kwa makosa mengine ya maadili mradi kuondolewa huku kusipelekee kubadilishwa kwa usajili wake (soma **Adabu inayopelekea Kubadilishwa kwa Usajili** hapa chini).

Kwa siku yoyote **ya kuondolewa zaidi ya siku 10 za shule katika mwaka mmoja** ambayo haipelekei kubadilishwa kwa usajili, wahudumu wa shule, kwa ushauri wa angalau mmoja wa wanafunzi wa mtoto, sharti wabaini kiwango ambacho huduma zinahitajika, kumwezesha mtoto kuendelea kutumia mtaala wa jumla wa elimu, ingawa katika mazingira tofauti anaendelea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto huyu. Utawala wa shule sharti umpe mtoto wako huduma zinazobainishwa na wahudumu wa shule kwa kushauriana na angalau mmoja wa walimu wa mtoto.

Wahudumu wa shule wanaweza kuagazia hali yoyote maalum kwa kuzingatia kesi moja baada ya nyingine ili kubaini ikiwa mtoto wako anafaa kubadilishiwa usajili anapokiuka maadili ya mwanafunzi. Wakati wa kufanya uamuzi wa kesi baada nyingine ikiwa mtoto anafaa kuadhibiwa kwa kubadilishiwa usajili, mambo kama vile historia ya nidhamu ya mtoto, uwezo wa kuelewa athari, kuomba msamaha na usaidizi anaopewa mtoto wako kabla ya kukiuka maadili ya shule yanaweza kuchangia hali maalum itakayoangaliwa na wahudumu wa shule.

Ufafanuzi wa Hali Maalum

34 CFR 300.530(i)

- Dawa inayodhibitiwa inamaanisha dawa au kemikali nyingine yoyote inayotambuliwa katika **SDCL** 34-20B-11 hadi 34-20B-26, inayojumuisha, au sehemu za I, II, III, IV, or V katika ibara ya 202(c) ya Kanuni ya Dawa Inayodhibitiwa 21 U.S.C. 812(c)).
- Dawa za kulevya inamaanisha dawa inayodhibitiwa; lakini haijumuishi dawa inayodhibitiwa ambayo inakubaliwa kisheria au inayotumiwa kwa ushauri wa ntaalamu wa afya aliye na leseni au inayomilikiwa au kutumiwa kwa mujibu wa sheria katika mamlaka mengine yoyote kwenye **SDCL** 34-20B-11 hadi 34-20B-26, inayojumuisha, au katika kipengele kingine chochote cha sheria ya Jimbo.
- Jeraha baya la mwili inamaanisha inayopewa dhana “jeraha baya la mwili” katika aya ya (3) ya sehemu ndogo ya (h) ya sehemu ya 1365 ya mada ya 18, katika Maadili ya Marekani.
- Dhana jeraha mbaya la mwili inamaanisha jeraha linalosababisha—
 - Uwezekano mkubwa wa kufa;
 - Maumivu makali ya kimwili
 - Kiungo cha mwili kuharibika kwa muda mrefu; au
 - Kupoteza au kulemaa kwa

Mabadiliko ya Usajili kutokana na Utovu wa Nidhamu

34 CFR 300.536, 34 CFR 300.530(h) ARSD 24:05:26:02.01; 34 CFR 300.530(h)

Kumwondoa mtoto wako kutoka eneo alikosajiliwa sasa ni **badiliko la usajili** ikiwa:

1. Kuondolewa huku ni kwa zaidi ya mfululizo wa siku 10 za shule; **au**
2. Au mtoto wako ameondolewa mara kadhaa kwa namna ambayo inafuata mtindo fulani kwa sababu:
 - a. Mfuatano wa kuondolewa umezidi siku 10 za shule katika mwaka mmoja;
 - b. Tabia ya mtoto wako inafanana kabisa na tabia yake katika matukio ya awali yaliyosababisha kuondolewa mara kadhaa; **na**
 - c. Mambo mengine kama vile kipindi cha kila kuondolewa, jumla ya muda wa kuondolewa na jinsi kuondolewa huku kunavyokaribiana.

Utawala wa shule huamua ikiwa mtindo wa kuondolewa unasababisha kubadilika kwa usajili kwa mujibu wa kila kesi. Utawala wa shule unapoamua kumwondoa mtoto wako kwa sababu ya kukiuka maadili kwa namna ambayo itapelekea kubadilika kwa usajili, utawala huu sharti ukujulisha siku hiyo hiyo na ukupe ilani ya utaratibu wa kukulinda.

Uamuzi huu wa ikiwa kuondolewa kutasababisha kubadilika kwa usajili unaweza kukaguliwa kwa kufuata utaratibu wa mchakato yakinifu wa kusikiliza kesi na kufikishwa mahakamani.

Sharti mkutano wa Timu ya IEP ufanywe ili kutekeleza Uamuzi Dhihirisho kabla ya kutoa adhabu ya kubadilisha usajili wa mtoto wako.

utendakazi wa sehemu, kiungo cha mwili, au ubongo.

- Silaha inamaana inayopewa dhana ya “silaha hatari” katika aya ya (2) ya sehemu ndogo ya kwanza (g) ya sehemu ya 930 ya mada ya 18, katika Maadili ya Marekani.
- Dhana silaha hatari inamaanisha silaha, kifaa, ala, kitu chenye uhai au kisicho na uhai, kinachotumika, au inayoweza kusababisha, mauti au majereha mabaya katika mwili, isipokuwa dhana hii haijumuishi kisu cha mfukoni chenye ncha inayopungua urefu wa inchi 2 1/2.

Dhihirisho Uamuzi na Matokeo Yanayotarajiwa

34 CFR 300.530(c) and (e); ARSD 24:05:26:09.03; 34 CFR 300.531; ARSD 24:05:26:09.02

Ndani ya siku 10 za shule za uamuzi wowote wa kubadilisha usajili wa mtoto wako kwa sababu ya kukiuka maadili ya mwanafunzi, timu ya IEP ya mtoto wako (kama unavyobainisha na wewe na utawala wa shule) sharti ikague maelezo yote muhimu katika faili ya mtoto wako, ikijumuisha IEP yake, maoni yoyote ya mwalimu na maelezo yoyote unayotoa ili kubaini:

1. Ikiwa utovu huo wa nidhamu umesababishwa na, au ulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja, na ulemavu wa mtoto wako; **au**
2. Au utovu huu wa nidhamu umetokana moja kwa moja na utawala wa shule kukosa kutekeleza IEP ya mtoto wako.

Ikiwa Timu ya IEP ya mtoto itabaini kuwa (1) au (2) yaliyo hapo juu yametimizwa, basi utovu huu ni dhihirisho wa ulemavu wa mtoto wako.

Ikiwa ukiukaji wa maadili ulikuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto wako, utawala wa shule sharti uchukue hatua za haraka kutatua ulemavu huu. Isitoshe, Timu ya IEP sharti:

1. Ifanye **tathmini ya utendakazi (FBA)**, isipokuwa ikiwa utawala wa shule umefanya FBA na kutekeleza **mpango wa kurekebisha tabia (BIP)** ya mtoto wako; **au**
2. Ikiwa tayari BIP imebuniwa, kuikagua na kuiboresha, inavyohitajika, kurekebisha tabia; **na**
3. Isipokuwa inavyobainishwa katika “hali maalum” (yaani silaha, dawa za kulevya, jeraha mbaya la mwili) mtoto wako sharti arudishwe kwenye usajili wake wa awali, isipokuwa unapokubaliana na utawala wa shule kubadilisha usajili kama sehemu ya kuboresha BIP ya mtoto wako.

Tafadhali kumbuka: Mtoto wako sharti afuate nidhamu na kanuni sawa kama zinazofuatwa na mwanafunzi yeyote shuleni na ataendelea kupokea huduma zinazofanuliwa katika IEP, lakini huenda huduma hizi zisiwe katika eneo moja.

Ikiwa ukiukaji wa maadili haukuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto wako, huenda mtoto akaadhibiwa kwa njia hii hii na kwa muda unaotumiwa kuwaadhibu wanafunzi wasio na ulemavu (isipokuwa sharti mtoto wako ahudumiwe) Kwa kuwa kuondolewa ni kubadilisha usajili, Timu ya IEP sharti:

1. Ihakikishe kuwa mtoto wako anapokea huduma na maboresho, FBA, marekebisho ya tabia , yaliyobuniwa ili kuzuia ukiukaji wa tabia kutokea tena;
2. Ibaini huduma za kumpa mtoto wako, kumwezesha kuendelea kuhusika katika mtaala wa jumla wa elimu, ingawa katika mazingira tofauti na kuendelea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto wako; **na**
3. Kuamua mazingira ya muda ya elimu ya kumpa mtoto wako huduma.

Hali Maalum na Matokeo yanayotarajiwa

34 CFR 300.530(g); 34 CFR 300.531; ARSD 24:05:26:09.02

Hata ikiwa tabia ya mtoto wako imebainiwa kuwa dhihirisho la ulemavu wake, wahudumu wa shule wanaweza kumwondoa na kumpeleka katika mazingira ya muda ya elimu (IAES) kwa muda usiozidi **siku 45 za kazi, ikiwa mtoto wako:**

1. Amebeba silaha au ana silaha shuleni, katika majengo ya shule au katika hafla ya shule;
2. Anamiliki au kutumia dawa za kulevya, au anauza au anachangia kuuza dawa inayodhibitiwa, akiwa shuleni, katika majengo ya shule au katika hafla ya shule; **au**
3. Amemjeruhi mtu mwingine mwilini akiwa shuleni, katika majengo ya shule au katika hafla ya shule.

Kabla ya kubadilisha usajili wa mtoto kutokana na hali hizi maalum, Timu ya IEP sharti:

1. Ihakikishe kuwa mtoto wako anapokea huduma na maboresho, FBA, marekebisho ya tabia , yaliyobuniwa kuzuia ukiukaji wa tabia kutokea tena;
2. Ibaini huduma za kumpa mtoto wako, kumwezesha kuendelea kuhusika katika mtaala wa jumla wa elimu, ingawa katika mazingira tofauti na kuendelea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto wako; **na**
3. Kuamua mazingira ya muda ya elimu ya kumpa mtoto wako huduma.

Ikiwa tabia hii imebainishwa kuwa si dhihirisho la ulemavu wa mtoto wako, huenda mtoto akaadhibiwa kwa njia na muda sawa unaotumiwa kuwaadhibu wanafunzi wasio na ulemavu kama inavofafanuliwa hapa juu katika Ubainishaji wa Dhihirisho.

Kwa maelezo zaidi katika masuala yaliyo hapo juu, tafadhali angalia ufafanuzi kwenye Kiambatisho.

Mchakato yakinifu wa Kusikiliza malalamishi kuhusu Kuwaadhibu Wanafunzi wenye Ulemavu

34 CFR 300.532(a); ARSD 24:05:26:09.06; 34 CFR 300.532(b); ARSD 24:05:26:08.02; 34 CFR 300.532(c); ARSD 24:05:26:09.08; 34. CFR 300.533; ARSD 24:05:26:09.07

Ikiwa hukubaliani na uamuzi wowote unaohusu kubaini dhihirisho **au** kumsajili mtoto wako kwa mujibu wa utaratibu wa nidhamu katika IDEA, unaweza kuomba kusikizwa kwa kupiga ripoti ya mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi.

Isitoshe, ikiwa utawala wa shule unaamini kuwa kudumisha usajili wa sasa wa mtoto wako kutapelekea kuwepo kwa ajali kwa mtoto wako au watoto wengine, utawala **unaweza** kuomba kusikizwa kwa kupiga ripoti ya mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi.

Afisa anayesikiliza kesi anasikiza na kufanya uamuzi kutokana na, rufaa iliyoombwa kwa mujibu wa sehemu ya kukata rufaa ya nidhamu ya IDEA. Afisa anayesikiliza kesi anaweza:

1. Kumrudisha mtoto wako aliposajiliwa hapo awali ikiwa atabaini kuwa kuondolewa huku kulikiuka utaratibu wa nidhamu au kuwa tabia ya mtoto wako ilikuwa dhihirisho ya ulemavu wake; **au**
2. Kuamuru mabadiliko ya usajili wa mtoto wako hadi kwa mazingira ya elimu yanayofaa kwa muda usiozidi siku 45, ikiwa afisa anayesikiliza kesi atabaini kuwa mtoto wako huenda akajeruhiwa au akawajeruhi wengine ikiwa atasalia katika usajili uliopo.

Utawala wa shule unaweza kurudia tena mchakato wa kuomba kusikizwa ili kuongeza muda wa kubadilisha usajili kwa siku zingine 45 za kipindi cha shule ikiwa utawala huu unaamini kuwa mtoto wako ana uwezo mkubwa wa kujijeruhi au kuwajeruhi wanafunzi wengine ikiwa atarejeshwa kwa usajili wa awali.

Kila ombi la kusikizwa linapotumwa kwa mujibu wa kifungu cha kukata rufaa dhidi ya adhabu katika IDEA, wewe au utawala wa shule unaohusika katika mzozo mna fursa ya kusikizwa kwa haraka bila ubaguzi. Huu unajulikana kama **utaratibu wa kusikizwa kwa haraka**.

Afisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo ina jukumu la kumteua hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo bila ubaguzi wowote. Hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo ana jukumu ya kupanga utaratibu wa kusikizwa kwa haraka, ambao sharti ufanyike ndani ya siku 20 za shule kuanzia tarehe ambayo ombi la kusikizwa lilitumwa. Afisa anayesikiliza kesi sharti afanye uamuzi ndani ya siku 10 za shule baada ya tarehe ya kusikiza kesi.

Isipokuwa wewe na wilaya ya shule mkubaliane kuiondoa kwa kuandikia Mkutano wa kufanya Uamuzi, au kutumia mchakato wa upatanisho:

1. Mkutano wa Uamuzi sharti ufanyike ndani ya siku saba baada ya kupokea ilani ya mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi; **na**
2. Mchakato yakinifu wa kusikiliza kesi unaweza kuendelea isipokuwa ikiwa suala hili limetatuliwa ndani ya siku 15 baada ya kupokea malalamishi ya kusikizwa.

Wewe au utawala wa shule mnaweza kukata rufaa kwa uamuzi wa hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo katika kesi zinazosikizwa haraka jinsi tu unavyokata rufaa dhidi ya uamuzi katika kesi zingine za kawaida.

Mzazi au utawala wa shule unapomba kusikizwa kwa mujibu wa sehemu ya kukata rufaa ya IDEA, mtoto sharti asalie katika **Mazingira Mbadala ya Muda wa Kielimu** hadi rufaa itakaposhughulikiwa isipokuwa panapokuwa na hali maalum na au wewe na shule mnapokubaliana vinginevyo.

Ulinzi wa Watoto Wasiobainishwa Kustahiki kwa Elimu ya Walio na Ulemavu na Huduma Husika

34 CFR 300.534; ARSD 24:05:26:14

Mtoto ambaye amekiuka maadili lakini bado hajabainishwa kustahiki elimu kwa watu walio na ulemavu na huduma kama hizi anaweza kudai yoyote kati ya ulinzi wa IDEA, ikiwa utawala wa shule ulifahamu kuwa mtoto huyu huenda akawa na ulemavu.

Kwa makusudi ya kuendeleza ulinzi wa IDEA, utawala wa shule unachukuliwa kufahamu kuwa mtoto ana uwezo wa kuwa na ulemavu kabla ya tabia iliyopelekea kuadhibiwa ikiwa:

1. Ikiwa uliandikia wasimamizi, viongozi au mwalimu wa mtoto wako kuonesha malalamishi yako, kuwa mtoto wako anahitaji elimu ya walemavu na huduma kama hizi;
2. Uliomba mtoto wako kutathminiwa; **au**
3. Mwalimu wa mtoto wako, au wahudumu wengine wa shirika la elimu katika eneo lako, walimlalamikia mkurugenzi wa elimu kwa watu walio na ulemavu katika utawala wa shule au kwa wasimamizi wengine wa utawala huu kuhusu mtindo wa tabia unaodhihirishwa na mtoto wako.

Utawala wa shule hautachukuliwa kujua kuwa mtoto wako ana ulemavu ikiwa hukuiruhusu imtathmini au ulikataa kutoa idhini ya mtoto wako kupokea elimu ya watu walio na ulemavu au huduma kama hizi katika Sehemu ya B ya IDEA, au mtoto wako ametathminiwa hapo awali na kubainishwa kuwa ana ulemavu kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA.

Ikiwa utawala wa shule haukuwa unafahamu kuwa mtoto wako alikuwa na ulemavu kabla ya kumwadhibu, basi hatalindwa na IDEA. Badala yake, hatua za mara kwa mara ya adhabu ambazo watoto wasio na ulemavu hupokea baada ya kukiuka maadili yatatumika kwa mtoto wako. Hata hivyo, ikiwa wewe au utawala wa shule umetuma ombi la kutathmini mtoto wako katika kipindi cha adhabu, tathmini hii sharti ifanywe na utawala wa shule kwa haraka. Katika kipindi hiki cha **tathmini kufanywa kwa haraka**, hadi tathmini ikamilike, mtoto wako atasalia katika usajili utakaobainishwa na mamlaka ya shule, ambao unaweza kujumuisha kufukuzwa kwa muda au kuondolewa kabisa bila kupokea huduma za elimu. Kutokana na maelezo ya tathmini ambayo wewe na utawala wa shule mmetoa, ikiwa mtoto wako hatimaye atabainishwa kuwa na ulemavu, utawala huu sharti umpe elimu ya walio na walemavu na huduma kama hizi kwa mujibu wa vipengele vyote vya Sehemu ya B ya IDEA ikijumuisha sheria za nidhamu na masharti ya FAPE.

UTARATIBU WA KUTATUA MZOZO KATIKA JIMBO

Malalamishi ya Jimbo

34 CFR 300.151; ARSD 24:05:15:02; 34 CFR 300.153; ARSD 24:05:15:03; 34 CFR 300.152; ARSD 24:05:15:05

Malalamishi dhidi ya jimbo ni taarifa iliyoandikwa kwa kutiwa saini na mtu au shirika, ikijumuisha malalamishi kando na ya jimbo, yanayodai kuwa Idara ya Elimu ya South Dakota, Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo au utawala wa shule umekiuka masharti ya Sehemu ya B ya IDEA au inatekeleza amri, sheria au kanuni ya jimbo au shirikisho zinazotumika katika mipango ya elimu ya watu wenye ulemavu. Malalamishi haya sharti pia yajumuishe ukweli wa hali.

	Malalamishi ya Nchi
Yanapotumika	Malalamishi ya Nchi huandikwa inapoaminika kuwa shirika au utawala wa shule wa umma umekiuka IDEA na malalamishi yenyewe yanaomba Shirika la Elimu Nchini (SEA) kufanya uchunguzi.
Anayeweza kulalamika	Mtu au shirika lolote linaweza kuandika malalamishi ya nchi.
Jinsi ya kuandika	Mtu au shirika linaloandika malalamishi dhidi ya Jimbo sharti litume nakala ya malalamishi haya kwa utawala wa shule unaomhudumia mtoto na pia kutuma malalamishi haya kwa Ofisi ya Elimu ya Walio na Ulemavu katika Jimbo. Ofisi ya Elimu ya Walio na Ulemavu katika Jimbo imebuni mfano wa fomu ya kusaidia wazazi na watu wengine katika kujaza malalamishi yao dhidi ya jimbo; ingawa, huhitajiki kutumia fomu hii ya mfano. Unaweza kutumia mfano wa fomu unaofaa au fomu au hati nyingine, mradi fomu au hati inayotumika inatimiza masharti ya maudhui ya kujaza malalamishi ya Nchi. Unaweza kupata fomu za kukuongoza kwenye https://doe.sd.gov/sped/complaints.aspx .
Matokeo au Yanayotarajiwa	Uamuzi ulioandikwa na unaojumuisha matokeo, hitimisho na uamuzi ulioafikiwa. Inajumuisha pia hatua za marekebisho ambazo sharti wilaya ichukue, panapohitajika.
Manufaa	Uamuzi wa kuandikwa ndani ya siku 60 za kazi baada ya kujaza fomu, isipokuwa muda unapoongezwa. Ni rahisi sana kujaza fomu ya malalamishi ya nchi. Ikiwa matokeo yametolewa, masuala ya mwanafunzi binafsi au ya wilaya pana yanaweza

	kubadilishwa.
Muamuzi	Nchi ina jukumu la kuhakikisha kuwa uchunguzi umekamilika na ripoti kamili kutolewa.
Kipindi cha Muda cha kujaza fomu, mkutano na uamuzi	<p>Malalamishi sharti yawe na madai ya ukiukaji uliotokea muda usiozidi mwaka mmoja kabla ya tarehe ya malalamishi kupokewa na idara.</p> <p>Uamuzi wa kuandikwa sharti utolewe ndani ya siku 60 za kazi kuanzia tarehe ya kujaza fomu ya malalamishi, isipokuwa kipindi hiki cha muda kinapoogezwa (nyongeza haiwezi kuzidi siku 30).</p>
Unapaswa kujumuisha maelezo yepi kwenye ombi?	<ol style="list-style-type: none"> 1. Taarifa ya kuonesha kuwa Idara ya Elimu ya South Dakota, Mipango ya Elimu ya Walio na Ulemavu katika Jimbo au utawala au shule umekiuka masharti ya Sehemu ya B ya IDEA au unatekeleza amri, sheria au kanuni ya jimbo au Nchi zinazotumika katika mipango ya elimu ya Walio na Ulemavu; 2. Ukweli ambao taarifa unaegemea; 3. Saini na anwani ya mawasiliano ya mlalamishi; na 4. Ikiwa unadai ukiukaji unaomhusu mtoto mahususi: <ol style="list-style-type: none"> (a) Jina na eneo anapoishi mtoto huyu; (b) Jina la shule anakosomea mtoto huyu; (c) Katika hali inayomhusu mtoto au kijana asiye na makazi (katika maana ya sehemu ya 725(2) ya Kanuni ya the McKinney-Vento Homeless Assistance Act (42 U.S.C. 11434a(2)), anwani ya mtoto huyu na jina la shule anakosomea; (d) Ufafanuzi wa aina ya shida ya mtoto, ukijumuisha hoja zinazohusiana na shida; na (e) Pendekezo la utatuzi wa tatizo kwa kiwango kinachojulikana na anachoweza kutumia mlalamishi wakati wa kujaza fomu.
Nini hutokea baada ya kujaza fomu?	<p>Mkurugenzi wa Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo huteua mchunguzi wa malalamishi na washauri wowote wanaohitajika kuchunguza malalamishi.</p> <p>Mchunguzi anaweza kufanya uchunguzi huru kwa njia moja kwa moja, anapohitajika kufanya hivyo.</p> <p>Mchunguzi sharti amruhusu mlalamishi kuwasilisha maelezo ya ziada kando na yale yaliyoandikwa kwenye malalamishi ya Nchi, kwa njia ya mdomo au kuandika, tuhuma kwenye malalamishi.</p> <p>Mchunguzi ataruhusu utawala wa shule kujibu malalamishi, ikijumuisha, kwa kiwango cha chini kabisa:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kwa hiari ya utawala wa shule, kutoa pendekezo la kutatua malalamishi; na 2. Kumpa mzazi aliyeripoti malalamishi na utawala wa shule kwa hiari yao fursa ya kutumia mbinu ya upatanisho ili kupata utatuzi. <p>Mchunguzi atampendekezea Mkurugenzi wa Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo;</p> <p>Baada ya kukagua maelezo yote yanayohitajika, Mkurugenzi wa Mipango ya Elimu kwa</p>

	<p>Walemavu atafanya uamuzi wake ikiwa malalamishi ni sahihi, hatua ya marekebisho yanayohitajika kutatua malalamishi na kipindi cha muda ambacho hatua mwafaka inapaswa kukamilika. Mkurugenzi wa Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo atawasilisha ripoti iliyoandikwa ya uamuzi alioufikia kwa wahusika wote.</p> <p>Ripoti hii ya kuandikwa itaangazia kila tuhuma kwenye malalamishi, itakuwa na matokeo na uamuzi na kujumuisha sababu za kufikia uamuzi huo.</p> <p>Hati ya kuthibitisha hatua za urekebishaji zilizochukuliwa na utawala wa shule zitahifadhiwa kwenye Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Watu Walio na Ulemavu na kujumuishwa kwenye mchakato wa ufuatiliaji wa Jimbo.</p>
Mambo ya kuzingatia	<p>Suala haliwezi kuwa katika malalamishi ya Kitaifa na la kufuata mchakato yakinifu wa kusikilia malalamishi kwa wakati mmoja. Jambo hili likitokea, Taifa litaweka kando sehemu ya malalamishi yoyote dhidi ya Taifa yanayoshughulikiwa katika mchakato yakinifu wa kusikiliza kesi hadi uamuzi utakapofanywa. Masuala mengine yoyote katika malalamishi dhidi ya Taifa ambayo si sehemu ya mchakato yakinifu wa kusikiza malalamishi yatatatuliwa kwa wakati ufaao kupitia mchakato wa malalamishi dhidi ya Taifa.</p> <p>Ikiwa swali linaloulizwa katika malalamishi dhidi ya Taifa liliamuliwa hapo awali katika mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi na ambalo linahusu wahusika wale wale, uamuzi huo utatumika kwa pande zote na Ofisi ya Kitaifa ya Mipango ya Elimu kwa Walio na Ulemavu sharti imwarifu mlalamishi.</p> <p>Malalamishi kwa shirika la Kitaifa yanayodai kukosa kwa utawala wa shule katika kutekeleza uamuzi uliofanywa katika mchakato yakinifu wa kusikiza malalamishi sharti yatatuliwe na Ofisi ya Kitaifa ya Mipango ya Elimu kwa Walio na Ulemavu.</p>
Gharama	Hakuna gharama ya kujaza fomu

Upatanisho

34 CFR 300.506; ARSD 24:05.30.05

Makundi husika yanaweza kutatua mizozo inayohusu suala lolote katika kanuni za elimu kwa walio na ulemavu katika Jimbo kwa kufuata mchakato wa upatanisho.

Upatanisho unawapa uwezo bora, bila ugomvi wa kutatua mzozo kati ya wazazi na mifumo ya shule. Kupitia usaidizi wa mwezeshaji mwenye maarifa asiyebugua (mpatanishi) wahusika katika mzozo huhimizwa kuwasiliana kwa uwazi na heshima kuhusu tofauti zao na kufikia uamuzi. Uamuzi hufanywa na wahusika katika mchakato wa upatanisho.

Mchakato wa Upatanisho	
Wakati unapotumika	Wakati wowote wazazi na utawala wa shule wanapokosa kuelewana kuhusu elimu ya walio na ulemavu na huduma kama hizi.

	Sharti kila upande ukubali upatanisho. Ni ya hiari
Anayeweza kujaza fomu	Mzazi au Utawala wa Shule ya Umma
Jinsi ya kujaza	Mhusika anayetuma ombi la kuomba upatanisho anapaswa, kutuma barua pepe au faksi kwa Afisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo. Ofisi ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo imebuni mfano wa fomu ya kusaidia wazazi na watu wengine katika kutuma ombi la upatanisho; ingawa, huhitajiki kutumia fomu hii ya mfano. Unaweza kutumia mfano wa fomu unaofaa au hati nyingine. Unaweza kupata fomu za kukuongoza kwenye https://doe.sd.gov/sped/complaints.aspx .
Matokeo au Yanayotarajiwa	Buni mkataba wa kuandika, wenye sahihi ambao unakubalika katika mahakama yoyote ya Kitaifa au ya wilaya nchini Marekani.
Manufaa	Majadiliano hayafichuliwi na Mazungumzo hayawezi kutumiwa kama ushahidi katika mchakato yakinifu wa kusikiliza kesi. Sharti wewe na mwakilishi wa utawala wa shule aliyeidhinishwa kutia saina kwa niaba yake mtie saina kwenye mkataba.
Muamuzi	Mzazi na utawala wa shule wanashirikiana, wana uwezo wa kudhibiti matokeo na kupata suluhu.
Kipindi cha Muda cha kujaza fomu, mkutano na uamuzi	Inapatikana wakati wowote, hata ikiwa umepiga ripoti kwa taifa umeomba kuanzishwa kwa mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi. Sharti nchi ihakikishe kuwa kipindi cha upatanisho kimeratibiwa kwa wakati unaofaa na kufanywa katika eneo linalowafaa wahusika katika mzozo [§300.506(b)(5)].
Unapaswa kujumuisha maelezo yepi kwenye ombi?	Hakuna kanuni ya masharti; ingawa, unaweza kutumia mfano wa fomu iliyotajwa hapo juu kama mwongozo.
Nini hutokea baada ya kujaza fomu?	Upatanisho sharti ufanywe na mpatanishi mwenye ujuzi asiye na mapendeleo ambaye ana maarifa ya mbinu bora za upatanisho. Wapatanishi huchaguliwa bila kufuata utaratibu, kwa kubadilishana zamu, au mbinu nyingine isiyobagua. SEP huhifadhi orodha ya watu wanaostahiki na wenye ujuzi katika sheria na kanuni zinazohusu utoaji wa elimu kwa walemavu na huduma kama hizi. Kila kipindi katika mchakato wa upatanisho sharti kiratibiwe kwa wakati unaofaa na kufanywa katika eneo linalowafaa nyote wawili. Upatanisho ni mchakato usio rasmi, unaofanywa kwa muktadha usio na ugomvi.
Mambo ya kuzingatia	Upatanisho haupaswi kutumiwa kumnyima au kuchelewesha haki ya mzazi ya kusikilizwa mahakamani au kumnyima haki zingine zinazotolewa katika Sehemu ya B ya IDEA.

	Ukiamua kutotumia mchakato wa upatanisho, Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo au utawala wa shule unaweza kukupa fursa ya kukutana, kwa wakati na eneo linalokufaa, na mtu mwingine asiyehusika, kuhimiza utumiaji na kukufafanulia manufaa ya, kutumia mchakato wa upatanisho. Mhusika huyu ana kandarasi na kituo cha mafunzo na maelezo kwa wazazi au kituo cha kuwapa wazazi nyenzo katika jumuiya iliyobuniwa katika nchi au katika taasisi mbadala ya kutatua mizozo.
Gharama	Nchi itagharamia mchakato wa upatanisho, ikijumuisha mikutano na mtu asiyehusika.

Mchakato Yakinifu wa Kusikizwa kwa Malalamishi

34 CFR 300.507; 34 CFR 300.508-509; ARSD 24:05:30:07.01

Wewe au utawala wa shule mnaweza kutuma ombi la mchakato wa kusikizwa kwa kuomba kusikizwa katika suala lolote linalohusu, utambulisho, tathmini, usajili wa kielimu au sheria ya FAPE kwa mtoto wako.

Kusikizwa Bila Kubaguliwa Mahakamani

34 CFR 300.511-515; ARSD 24:05:30:09.04

Kila ombi la mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi linapopokewa, ikijumuisha malalamishi yanayohusu utaratibu wa nidhamu, isipokuwa linapotatuliwa kwa ukamilifu kabla ya wakati wa kusikizwa kufika, wewe au utawala wa shule unaohusika katika mzozo sharti muwe na fursa ya kusikizwa. Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo ina jukumu la kuhakikisha mchakato wa kusikizwa umefanyika bila ubaguzi.

Mchakato Yakinifu wa Kusikizwa kwa Malalamishi	
Wakati unapotumika	Yanatumika kutatua mizozo inayohusu, utambulisho, tathmini, usajili au sheria ya FAPE.
Anayeweza kujaza fomu	Mzazi au utawala wa shule unaweza kutuma ombi la kuomba mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi. Wakili au mtetezi kwa niaba ya mzazi au utawala wa shule ya umma.
Jinsi ya kujaza	Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo imebuni mfano wa fomu ya kusaidia wazazi na utawala wa shule kuomba ilani ya mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi. Haupaswi kutumia fomu za mifano. Mhusika anayeomba mchakato wa kusikizwa anaweza kutumia mfano wa fomu unaofaa au fomu au hati nyingine, mradi fomu au hati inayotumika inatimiza, masharti ya maudhui ya kujaza malalamishi ya kusikizwa.

	<p>Unaweza kupata fomu za kukuongoza kwenye https://doe.sd.gov/sped/complaints.aspx.</p> <p>Mhusika anayetuma ombi la mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi sharti atume nakala ya malalamishi haya kwa Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo.</p> <p>Malalamiko kuhusu mchakato wa kesi sharti yajumuishe maelezo yafuatayo:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Jina la mtoto; 2. Anwani ya anapoishi mtoto; 3. Jina la shule anakosomea mtoto; 4. Katika hali inayomhusu mtoto au kijana asiye na makazi (katika maana ya sehemu ya 725(2) ya Kanuni ya the McKinney-Vento Homeless Assistance Act (42 U.S.C. 11434a(2)), anwani ya mtoto huyu na jina la shule anakosomea; 5. Ufafanuzi wa aina ya shida ya mtoto, unaohusu pendekezo au uanzishaji au mabadiliko yaliyokataliwa, ikijumuisha hoja zinazohusiana na shida; na 6. Pendekezo la utatuzi wa shida. <p>Wewe au utawala wa shule hamtaweza kusikizwa hadi mhusika anayeomba kusikizwa atakapowasilisha malalamishi ya kusikizwa yanayotimiza masharti ya IDEA sehemu ya B yaliyoorodheshwa hapo juu.</p>
<p>Haki za Mhusika katika Kusikizwa kwa Kesi</p>	<p>Haki za Kusikizwa - ARSD 24:05:30:12</p> <p>Kila mhusika wakati wa kusikizwa ana haki ya:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kuambatana na kushauriwa na wakili na watu walio na maarifa au mafunzo maalum yanayohusu matatizo ya watoto walio na ulemavu isipokuwa kwamba hakuna mhusika anayeweza kuwakilishwa na mtu ambaye si wakili wakati wa kusikilizwa kwa kesi; 2. Kutoa ushahidi na kukabili, kuhoji na kuchochea mashahidi katika kuhudhuria; 3. Kukataa ujumuishaji wa ushahidi katika kusikizwa kwa kesi ambao hakuoneshwa angalau siku 5 za kazi kabla ya kusikizwa kwa kesi; 4. Kupokea rekodi iliyoandikwa, au, ukitaka, ya kielektroniki, neno kwa neno ya kusikizwa kwa kesi; na 5. Kupokea matokeo kwa kuandikwa, au, ukitaka matokeo ya kielektroniki na maamuzi. <p>Ufichuzi Zaidi wa Maelezo - ARSD 24:05:30:12.01</p> <p>Angalau siku tano za kazi kabla ya kusikizwa kwa kesi, wewe na utawala wa shule mtafichuliana tathmini zote zilzizofanywa kufikia tarehe hiyo na mapendekezo kutokana na tathmini ambazo wewe au utawala wa shule unanuia kutumia wakati wa kusikizwa kwa kesi.</p> <p>Afisa anayesikiliza kesi anaweza kutupilia mbali tathmini au pendekezo wakati wa kusikizwa kwa kesi kwa kukosa kutimiza masharti ya ufichuzi.</p>

	<p>Haki za Wazazi katika Kusikizwa kwa Kesi</p> <p>Kama mzazi anayehusika katika kesi, una haki ya:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kumwasilisha mtoto ambaye kesi yake inasikizwa; 2. Kuruhusu umma kusikiza kesi; na 3. Kupata rekodi za kusikizwa kwa kesi na matokeo ya hoja na uamuzi uliotolewa bila kutozwa ada yoyote.
<p>Matokeo au Yanayotarajiwa</p>	<p>Uamuzi uliondikiwa wa utambuzi wa ukweli, hitimisho ya sheria na hatua za marekebisho ambazo sharti wilaya ichukue ikiwa zinatumiwa.</p>
<p>Manufaa</p>	<p>Kuanzia tarehe ya kutuma ombi la mchakato wa kusikizwa kwa kesi mtoto anasalia katika shule aliposajiliwa isipokuwa mzazi na utawala wa shule ya umma wanapoamua vinginevyo.</p> <p>Uamuzi huu unawaunganisha wahusika wote wawili.</p> <p>Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo ina jukumu la kuhakikisha kuwa uamuzi huu umefuatwa, isipokuwa rufaa inapokatwa.</p>
<p>Muamuzi</p>	<p>Maamuzi ya Kusikizwa - ARSD 24:05:30:10.01</p> <p>Uamuzi wa afisa anayesikiliza kesi kuwa mtoto hakupewa FAPE sharti utokane na ithibati ya kutosha isipokuwa utaratibu wa ukiukaji huu unatimiza kigezo cha kutopewa FAPE.</p> <p>Katika maswala ya tuhuma za ukiukaji wa utaratibu, afisa anayesikiliza kesi anaweza kuamua kuwa mtoto wako hakupokea FAPE ikiwa upungufu wa utaratibu:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Unazuia haki ya mtoto wako kupata FAPE; 2. Unazuia pakubwa fursa yako ya kuhusika katika mchakato wa uamuzi wa IEP kuhusu kumpa mtoto wako FAPE; au 3. Umefanya mtoto wako kutopokea manufaa ya kielimu. <p>Hakuna maelezo katika sehemu hii yatakayofasiriwa kumzuia hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo kuamrisha utawala wa shule kuzingatia utaratibu wa masharti ya IDEA.</p> <p>Afisa Anayesikiliza Kesi Bila Ubaguzi - ARSD 24:05:30:10</p> <p>Afisa anayesikiliza kesi sharti:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Asiwe na mapendeleo (yaani asiwe ni mwajiriwa katika Idara ya Elimu ya South Dakota au katika utawala wa shule ya eneo lake na asiwe na maslahi ya kibinafsi au kitaalam yasiyokinzana na malengo ya kusikiza kesi); 2. Awe na maarifa, na uwezo wa kuelewa, sheria ya IDEA, kanuni za Jimbo au Kitaifa zinazohusu IDEA na ufasiri wa kisheria wa IDEA katika mahakama ya Jimbo na Kitaifa; 3. Ana maarifa na uwezo wa kusikiliza kesi kwa mujibu wa utaratibu unaofaa, unaohitajika kisheria; 4. Ana maarifa na uwezo wa kufanya na kuandika uamuzi kwa mujibu wa utaratibu unaofaa, unaohitajika kisheria;

	<p>Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo na utawala wa shule utahifadhi orodha ya watu wanaohudumu kama hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo. Orodha hii sharti iwe na taarifa ya kustahiki kwa kila mmojawapo wa watu hao.</p>
<p>Kipindi cha Muda cha kujaza fomu, mkutano na uamuzi</p>	<p>Kesi ya kusikizwa sharti iwe na tuhuma ya ukiukaji uliofanywa kwa muda usiozidi miaka miwili kabla ya taraha ambayo wewe au (utawala wa shule unaoomba kusikizwa) mlifua au mlipaswa kujua kuhusu tuhuma dhidi ya mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi. Kipindi kinachofafanuliwa hapo juu hakikatumiwa kwako ikiwa umezuiwa kuomba mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi kwa sababu ya:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Ufasiri mbaya na mahususi wa utawala wa shule kuwa ulitatu tatizo hilo; au 2. Utawala wa shule kutokuonesha maelezo yanayofaa kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA. <p>Vipindi vya Kusikizwa</p> <p>Muda usiozidi siku 45 baada ya kipindi cha utatuzi wa siku 30 kuisha au kubadilika kwa kipindi cha muda, panapohitajika, Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu itahakikisha kwamba:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Uamuzi umefanywa katika kusikiliza kesi; na 2. Wewe na utawala wa shule mmetumiwa nakala ya uamuzi huo. <p>Hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo anaweza kuongeza muda mahususi katika kipindi hiki cha muda wewe au utawala wa shule mnapotuma ombi.</p> <p>Kila kesi sharti isikizwe katika wakati na mahali panapokufaa wewe na mtoto husika.</p>
<p>Nini kitafanyikia huduma anazopokea mtoto wangu baada ya kujaza fomu?</p>	<p>Hali ya Mtoto Wakati wa Kusikizwa kwa Kesi (“Usihofu”) - 34 CFR 300.518; ARSD24:05:30:14</p> <p>Wakati wa mchakato wowote yakinifu wa kusikizwa kesi au kusikizwa kwa kesi mahakamani kuhusu kusikizwa kwa malalamishi, isipokuwa Ofisi ya Kitaifa ya Mipango ya Elimu kwa walio na Ulemavu au mnapokubaliana na utawala wa shule vinginevyo, mtoto anayehusika katika mchakato yakinifu wa kusikizwa atasajilia katika shule alikojiunga.</p> <p>Ikiwa unatuma ombi la kusajiliwa katika shule ya umma, mtoto wako, kwa kufuatia idhini yako, atasajiliwa kwenye ratiba ya shule hadi mchakato hii itakapokamilika.</p> <p>Ikiwa mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi unahusu ombi la huduma za awali katika Sehemu ya B ya mtoto anayehama kutoka Sehemu ya C ya IDEA hadi Sehemu B na hastahiki tena kupata huduma za Sehemu ya C kwa sababu amefikisha umri wa miaka mitatu, utawala wa shule hauhitajiki kutoa huduma za Sehemu ya C ambazo mtoto amekuwa akipokea.</p> <p>Ikiwa mtoto anastahiki elimu ya watu walio na ulemavu na huduma kama hizi katika Sehemu ya B na unakubali kipengele cha kwanza cha elimu kwa watu walio na huduma kama hizi, basi sharti utawala wa shule utoe elimu na huduma husika ambazo wewe na utawala wa shule hamzozanii.</p> <p>Mzazi au utawala wa shule unapooomba kusikizwa kwa mujibu wa sehemu ya kukata rufaa ya IDEA, mtoto sharti asalie katika Mazingira Mbadala ya Muda ya Kielimu hadi rufaa itakaposhughulikiwa isipokuwa panapokuwa na hali maalum na au wewe na shule</p>

	<p>mnapokubaliana vinginevyo.</p> <p>Ikiwa hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo anakubaliana nawe kuwa ni vyema kubadilisha shule, usajili huo sharti uchukuliwe kama mkataba kati yako na Ofisi ya Kitaifa ya Mipango ya Elimu Kwa Watoto wenye Ulemavu hadi kesi itakapokamilika.</p>
<p>Nini hutokea baada ya kujaza fomu?</p>	<p>Utoshelevu wa Malalamishi - ARSD 24:05:30:08.04</p> <p>Mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi utachukuliwa kuwa wa kutosha isipokuwa mhusika anayepokea mchakato huu, anapomwarifu hakimu wa kushughulikia masuala yanayohusu mizozo na mhusika mwingine kwa kuandika, ndani ya siku 15 za kupokea malalamishi ya kusikizwa, kwamba mhusika anayepokea anaamini kuwa mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi hautimizi masharti ya IDEA.</p> <p>Ndani ya siku tano baada ya kupokea hati hii, afisa anayesikiza kesi sharti afanye uamuzi ikiwa mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi unatimiza masharti ya IDEA na sharti awajulishe wahusika wote kwa kuwaandikia kuhusu uamuzi huo mara moja.</p> <p>Mhusika anaweza kurekebisha mchakato wake yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi ikiwa tu:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Mhusika mwingine anakubali marekebisho haya kwa kuandika na anapewa fursa ya kurekebisha mchakato wa kusikizwa kupitia Mkutano wa Uamuzi; au 2. Hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo hutoa idhini, isipokuwa kwamba anaweza tu kupeana idhini ya kufanya marekebisho kwa wakati wowote usiozidi siku tano kabla ya kesi kuanza kusikizwa. <p>Kipindi cha muda kitakachotumika katika mchakato wa kusikizwa kwa kesi kwa mujibu wa Sehemu ya B utaanza upya wakati mhusika atakapotuma ombi la marekebisho ya mchakato wa kusikiliza malalamishi, ikijumuisha kipindi cha Mkutano wa Uamuzi.</p> <p>Unaweza kutuma ombi la mchakato mwingine wa kusikizwa kwa malalamishi kando na ule ambao tayari umeomba wewe au utawala wa shule</p> <p><i>Jibu la Wilaya kwa Ombi la Mchakato wa Kusikizwa kwa Malalamishi Lililotumwa na Mzazi</i></p> <p>Ikiwa ni wewe unayeomba mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa kesi na utawala wa shule hujakutumia ilani ya kuandikwa mapema kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA kuhusu suala muhimu kwenye malalamishi yako, utawala wa shule, ndani ya siku 10 za kupokea ombi la mchakato yakinifu wa kusikiliza malalamishi, sharti ukutumie majibu yanayojumuisha:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Ufafanuzi wa sababu ya utawala wa shule kupendekeza au kukataa kuchukua hatua kwa ombi la mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi; 2. Ufafanuzi wa chaguo zingine ambazo Timu ya IEP ya mtoto wako ilikubali na sababu za kukataliwa kwa chaguo hizi; 3. Ufafanuzi wa kila utaratibu wa tathmini, ukaguzi, rekodi au ripoti ambayo utawala wa shule ulitumia kama sababu kuu ya hatua zilizo; na 4. Ufafanuzi wa mambo mengine yanayohusu hatua zilizopendekezwa au kukataliwa na utawala wa shule. <p>Jibu la utawala wa shule katika kifungu hiki halipaswi kuzuia utawala huu kuchukulia kuwa</p>

ombi lako la mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi halikuwa toshelevu.

Jibu la Mhusika Mwingine kwa Mchakato Yakinifu wa Kusikizwa kwa Malalamishi

Ikiwa utawala wa shule ndio unaoomba kusikizwa, mzazi anayepokea ombi la mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi sharti, ndani ya siku 10 za kupokea ombi hili, atumie utawala wa shule jibu linalojibu maswali yaliyoulizwa katika mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi.

Mkutano wa Uamuzi - 34 CFR 300.510; ARSD 24:05:30:08.12

Ikiwa ni wewe unayeomba mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi yako, ndani ya siku 15 za kupokea ilani ya malalamishi yako kusikizwa, na kabla ya kuanzishwa kwa mchakato huu, **utawala wa shule sharti** uitishe Mkutano wa Uamuzi ambao:

1. Unakujumuisha na wanachama husika wa Timu ya IEP walio na **ujuzi maalum** wa mambo yanayobainishwa kwenye mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi;
2. Unajumuisha mwakilishi wa utawala wa shule aliyeidhinishwa kufanya uamuzi kwa niaba ya utawala huu; **na**
3. Haujumuishi wakili wa utawala wa shule isipokuwa ukihudhuria pamoja na wakili wako.

Wewe na utawala wa shule mtaamua wanachama wa Timu ya IEP watakaohudhuria Mkutano wa Uamuzi.

Madhumuni ya Mkutano wa Uamuzi ni ili muweze kujadili malalamishi kutokana na ombi la mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi na mambo msingi katika malalamishi yako, ili utawala wa shule uwe na fursa ya kutatua mzozo ambao ndio chanzo cha ombi hili.

Mkutano huu wa Kutafuta Suluhu unahitajika isipokuwa:

1. Wewe **na** wiliaya ya shule mnapokubaliana kutupilia mbali mkutano huu kwa kuandika; **au**
2. Wewe na wiliaya ya shule mnapokubaliana kutumia mchakato wa upatanisho unaofafanuliwa kwenye hati hii.

Kipindi cha Siku 30 za Kutafuta Suluhu

Ikiwa utawala wa shule tayari umetatua malalamishi yako kwa kiwango cha kukuridhisha ndani ya siku 30 za kupokea ombi la mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi uliyotuma, mchakato wa kusikizwa kwa kesi unaweza kufanyika. Isipokuwa ilivyo hapa chini, kipindi cha muda wa kufanya uamuzi wa mwisho katika mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa kesi huanza baada ya kuisha kwa kipindi cha siku 30 za kufanya uamuzi.

Isipokuwa mnapokubaliana kuondoa Mkutano wa Uamuzi au kutumia upatanisho badala ya Mkutano huu, kukosa kwako kushiriki katika Mkutano huu kutachelewesha muda wa mchakato huu na kufanya uamuzi na ule wa kusikizwa kwa kesi hadi baada ya kufanyika kwa Mkutano wa Uamuzi.

Ikiwa utawala wa shule umeshindwa kujua ikiwa utashiriki katika Mkutano wa Uamuzi baada ya juhudi zao kunakiliwa, utawala huu wa shule unaweza, baada ya kukamilika kwa

	<p>kipindi cha siku 30 za kufanya uamuzi, kumwomba hakimu wa kushughuliki masuala ya mizozo kutupilia mbali ombi lako la mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi.</p> <p>Kunakiliwa kwa juhudi za utawala wa shule katika kukuomba kushiriki katika Mkutano wa Uamuzi sharti kujumuishe ithibati ya kujaribu kwa utawala wa shule kupangia kwa muda au mahali mlipokubaliana, kama vile:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au zilizojaribu kupigwa na matokeo ya simu hizo; 2. Nakala za mawasiliano ulizotumiwa na majibu yoyote uliyopokea; na 3. Rekodi ya kina ya ziara zilizofanywa nyumbani kwako au mahali pa kazi na matokeo ya ziara hizi. <p>Utawala wa shule usipofanya Mkutano wa Uamuzi ndani ya siku 15 baada ya kupokea ilani ya ombi lako la mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi yako au utawala huu unapokosa kushiriki katika Mkutano wenyewe, unaweza kumwomba hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo kuingilia kati ili aanzishe kipindi cha mchakato wa kusikizwa kwa kesi.</p> <p>Mabadiliko kwenye Kipindi cha Uamuzi cha siku 30 - ARSD 24:05:30:08.14</p> <p>Kipindi cha muda wa siku 30 za kufanya uamuzi kinabadilishwa na kipindi cha siku 45 za mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi kitaanza, siku baada ya matukio yafuatayo kutokea:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Wewe na wiliaya ya shule mnapokubaliana kwa kuandika kutupilia mbali Mkutano wa Uamuzi; 2. Baada ya upatanisho na Mkutano wa Uamuzi kuanza lakini kabla ya kuisha kwa kipindi cha siku 30, wewe na utawala wa shule mnapokubaliana kwa kuandika kuwa hataweza kuelewana; au 3. Mkikubaliana nyote wawili kwa kuandika kuendelea na upatanisho baada ya kipindi cha siku 30 kuisha, lakini baadaye, wewe au utawala wa shule mnapojiondoa kwenye mchakato wa upatanisho. <p>Mkataba wa Kufidia Ulioandikwa - ARSD 24:05:30:08.15</p> <p>Ikiwa suluhu ya mzozo itapatikana kwenye Mkutano wa Uamuzi wewe na utawala wa shule sharti muandike mkataba wa kisheria ambao:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Nyote wawili mmetia saini pamoja na mwakilishi wa utawala wa shule aliyeidhinishwa kutia saini kwa niaba ya utawala; na 2. Unaokubalika katika mahakama yoyote ya Kitaifa au ya wilaya nchini Marekani. <p>Wewe na wilaya ya shule mnapoandika mkataba katika Mkutano wa Uamuzi, wewe au utawala wa shule mnaoweza kughairi mkutano huu ndani ya siku 3 za kazi baada ya kutia saini kwenye mkataba.</p>
<p>Mambo ya kuzingatia</p>	<p>Jambo Muhimu katika Mchakato yakinifu wa Kusikizwa kwa Kesi - ARSD 24:05:30:09.05</p> <p>Wewe au utawala wa shule unaotuma ombi la mchakato wa kusikizwa kwa kesi hamwezi kuuliza maswali ambayo hamkuuliza wakati wa kusikizwa kwa malalamishi isipokuwa mmoja wenu anapokubali.</p>

	<p>Uamuzi huu ni wa kisheria, hata ikiwa hukubaliani nao.</p> <p>Rufaa ikitwa dhidi ya uamuzi, haitatekelezwa hadi rufaa ya mwisho itakapokatwa.</p> <p>Kwa kawaida utawala wa shule huwakilishwa na wakili.</p>
<p>Gharama</p>	<p>Shule sharti ikujulishe kuhusu huduma yoyote ya bila malipo au ya gharama ya chini na huduma zingine muhimu zinazopatikana katika eneo lako ikiwa:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Unaitisha maelezo haya; au 2. Wewe au utawala wa shule mnapotuma ombi la mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi <p>Mzazi atalipia gharama ya kupata huduma ya wakili. Angalia hapa chini uone maelezo zaidi kuhusu ada za wakili.</p>
<p>Maelezo zaidi</p>	<p>Uamuzi wa Mwisho</p> <p>Uamuzi unaofanywa baada ya kesi kusikizwa hauwezi kubadilishwa, isipokuwa kwamba mhusika yeyote anayehusika katika kesi anaweza kukata rufaa ya uamuzi huu kupitia hatua za kiraia.</p> <p>Hatua za Kiraia - 34 CFR 300.516; ARSD 24:05:30:11</p> <p>Mmoja wa wahusika katika mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa kesi (wewe au utawala wa shule) ambaye hajaridhishwa na matokeo na maamuzi ya hakimu wa kushughulikia masuala ya mizozo (ikijumuisha kusikizwa kwa kesi zinazohusu utaratibu wa nidhamu) ana haki ya kuchukua harakati ya kiraia kulingana na mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi. Hatua hii inaweza kuwasilishwa katika mahakama yoyote ya Kitaifa iliyo na mamlaka ya kusikiza aina hizi za kesi au mahakama ya wilaya nchini Marekani bila kujali kiasi cha utata.</p> <p>Mhusika anayewasilisha kesi hii ana siku 90 kuanzia tarehe ya uamuzi wa afisa anayesikiliza kesi kuomba idhini ya hatua za kiraia.</p> <p>Katika hatua za kiraia, mahakama:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Itapokea rekodi ya utaratibu wa usimamizi; 2. Itaangazia ushahidi zaidi wa mhusika yeyote anapooomba kufanya hivyo; na 3. Kukita maamuzi yake kwenye uzito wa ushahidi, itakubali ushahidi ambao itabaini kuwa unastahili. <p>Hakuna kipengele katika Sehemu ya B ya IDEA kinachozuia au kupunguza haki, utaratibu na suluhu zinazopatikana katika Katiba, Kanuni ya Wamerekani wenye Ulemavu ya 1990, sheria ya V ya Kanuni ya Urekebishaji ya 1973, au sheria nyingine ya Jimbo zinazolinda haki za watoto wenye ulemavu, isipokuwa tu kwamba kabla ya kuomba kuchukua hatua ya kiraia kwenye sheria hizi na kuomba kusikizwa tena ambako kunapatikana pia katika Sehemu ya B ya IDEA, utaratibu wa kutuma ombi la mchakato wa kusikizwa kwa malalamishi sharti ufuatwe kikamilifu kama tu ambavyo ingehitajika ikiwa hatua hii ingewasilishwa kwenye Sehemu ya B ya IDEA.</p> <p>Ada ya Wakili - 34 CFR 300.517; ARSD 24:05:30:11.01</p> <p>Katika hatua au utaratibu wowote unawekwa kwenye Sehemu ya B ya IDEA, mahakama,</p>

kwa uamuzi wake, inaweza kuwapa mawakili ada ambayo ungefaa kugharamia **ambayo utawala wa shule sharti ilipe**, ikiwa utashinda kesi.

Mkutano wa Uamuzi si mkutano unaoitishwa kutokana na usimamizi wa kusikiza kesi au hatua ya mahakama na pia haichukuliwi kuwa usimamizi wa kusikiza kesi au hatua ya mahakama kwa madhumuni ya kuwapa mawakili ada.

Mahakama, kwa uamuzi wake, inaweza kulipa mawakili ada zinazokubalika kama sehemu ya gharama ya Idara ya Kitaifa ya Mipango ya Elimu au utawala wa shule, ambayo **mahakama itamhitaji wakili wako kulipa**, wakili wako anapotuma ombi la mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi au hatua nyingine ya kuchukuliwa ambayo ni ya kipuzi, isiyoeleweka au isiyo na msingi, **au** ikiwa wakili wako aliendelea kushtaki baada ya mashtaka kuwa ya kipuzi, isiyoeleweka au isiyo na msingi.

Mahakama, kwa uamuzi wake, inaweza kulipa mawakili ada zinazokubalika kama sehemu ya gharama ya Idara ya Mipango ya Elimu katika Jimbo au utawala wa shule, ambao **mahakama inakuhitaji au wakili wako kulipa**, ikiwa ombi lako la mchakato wa kusikizwa kwa kesi au hatua nyingine ya kufuatwa iliwasilishwa kwa madhumuni mengine yasiyofaa, kama vile kusumbua, kusababisha kuchelewa, au kuongeza gharama ya mashtaka bila sababu.

Ukishinda kesi, mahakama itapunguza kiasi cha ada za wakili unayopewa kwa mujibu wa Sehemu ya B ya IDEA, mahakama ikigundua kwamba, wewe au wakili, wakati wa kesi kuendelea:

1. Mlichelewesha sana utatuzi wa mzozo;
2. Ada ya wakili wako imezidi sana ada ya kila saa inayotozwa na mawakili wengine katika jumuiya katika kutoa huduma kama hizi;
3. Muda uliotumia, na huduma za kisheria alizotoa wakili wako ni nyingi sana ikilinganishwa na aina ya utaratibu ; **au**
4. Wakili hakuipa shule maelezo yanayofaa kwenye mchakato yakinifu wa kusikizwa kwa malalamishi.

Vipengele hivi vya mapunguzo havitumiki katika hatua yoyote au utaratibu ikiwa mahakama itagundua kuwa Idara ya Elimu katika Jimbo au utawala wa shule ulichelewesha sana utatuzi wa mwisho wa hatua au utaratibu au kulikuwa na ukiukaji wa Sehemu ya B ya IDEA.

Matokeo na Uamuzi kwa Bodi ya Ushauri na Raia kwa Ujumla

Ofisi ya Mipango ya Elimu kwa Walemavu katika Jimbo, baada ya kufuta maelezo yoyote ya kukutambulisha, itatuma matokeo na uamuzi wa afisa anayesikiliza kesi kwa bodi ya Ushauri wa Kitaifa na kuhakikisha kuwa umma inaweza pia kuyapata.

UHAMISHAJI WA HAKI

Uhamishaji wa Haki za Wazazi katika Umri wa Wengi

34 CFR 300.520; ARSD 24:05:30:16.01

Mtoto aliye na ulemavu anapofikisha umri wa miaka kumi na nane, umri wa wengi (isipokuwa kwa mtoto mlemavu ambaye haki zake zimeondolewa au kukabidhiwa mhusika mwingine), haki zote katika Sehemu ya B ya IDEA huhamishwa kutoka kwako hadi kwa mtoto wako huyu isipokuwa kwamba utawala wa shule utakupa wewe na mtoto wako ilani yoyote inayohitajika kwa mujibu wa elimu kwa watoto walio na ulemavu.

Ikiwa mtoto wako amefungwa katika gereza ya watu wazima au la watoto, taasisi ya Kitaifa, au ya eneo lako la kufanyiwa marekebisho, haki zote katika Sehemu ya B ya IDEA huhamishwa kwa mtoto wako anapofikisha umri wa miaka 18, umri wa wengi wao.

Wilaya ya shule itakujulisha wewe na mtoto wako kuhusu uhamishaji wa haki.

Ikiwa, umezingatia sheria ya Kitaifa, mtoto anayestahiki ambaye haki zake hazijaondolewa au kukabidhiwa mhusika mwingine na mahakama anabainishwa **kutokuwa na** uwezo wa kutoa idhini inayofaa kwa mujibu wa mpango wake wa elimu, utawala wa shule utamteua mzazi, au ikiwa mzazi hayupo, mzazi mlezi ili kuwakilisha maslahi ya elimu ya mtoto huyu katika ustahiki wake katika Sehemu ya B ya IDEA.

UFUPISHO NA UFAFANUZI

ARSD – Kanuni za Usimamizi za South Dakota zinapatikana katika tovuti ya Dakota Legislature Legislative Research Council: <http://sdlegislature.gov/Rules/DisplayRule.aspx?Rule=24:05>.

Mpango wa Kurekebisha Tabia – au mapango wa kuhimiza tabia ambapo mwalimu hutumia kubadili tabia ya mwanafunzi na kudhibiti athari kwa kuchochea tabia nzuri.

Mtoto aliye na ulemavu – Mtoto aliye na ulemavu unamaanisha mtotoo aliyetathminiwa kwa mujibu wa §§300.304 hadi 300.311 kuwa na ulemavu wa kiakili, matatizo ya kusikia (ikijumuisha uziwi), matatizo ya kuzungumza au kunena, matatizo ya kuona (ikijumuisha upofu), usumbufu mkubwa wa kihisia (unaojulikana katika sehemu hii kama “usumbufu wa kihisia”), matatizo ya mifupa, tawahudi, jeraha mbaya kwenye ubongo, matatizo mengine ya kiafya, ulemavu fulani wa kimasomo, uziwi-upofu, ulemavu mbalimbali, na ambaye, kwa sababu hii, anahitaji elimu ya walio na ulemavu na huduma husika.

CFR – Kanuni za Maadili ya Jimbo

Idhini – Idhini baada ya kuarifiwa inamaanisha kuwa unapewa maelezo kamili kuhusu shughuli ambayo unahitajika kutoa idhini.

Siku – inamaanisha siku iliyo kwenye kalenda isipokuwa inapobainishwa vinginevyo kama siku ya kazi au ya shule.

Mchakato yakinifu – dhana ya kisheria inayoashiria utaratibu unaolinda haki ya mhusika. Katika elimu kwa watoto wenye ulemavu, kupewa mchakato yakinifu kunamaanisha kuwa utaratibu unaolinda haki ya mhusika unafuatwa na unafafanua pia mchakato wa kusikizwa kwa kesi ya usimamizi (yaani ‘Mchakato Yakinifu wa Kusikizwa kwa Malalamishi na ‘**Mchakato Yakinifu wa Kusikizwa kwa Kesi**’).

Kanuni ya Haki ya Elimu na Faragha ya Familia (FERPA) – ni sheria ya jimbo inayolinda faragha ya rekodi za elimu ya mwanafunzi.

Elimu Inayogharamiwa na Umma (FAPE) – Dhana ‘Free Appropriate Public Education’ au ‘FAPE’ inamaanisha elimu kwa walemavu na huduma husika ambazo: zinagharamiwa na utawala wa shule, kwa kusimamiwa na kuongozwa na umma na bila kutozwa ada; zinatimiza masharti ya **Shirika la Elimu ya Kitaifa (SEA)**; inajumuisha masomo katika shule ya chekechea, msingi, sekondari katika Nchi husika; na zinatolewa kwa kuzingatia mpango wa elimu ya kibinafsi (IEP)

Tathmini ya Uwezo wa Utendaji (FBA) – Mchakato wa kukusanya data ili kuweza kuelewa utendakazi (madhumuni) ya tabia ili kuweza kuandika mpango ufaao wa kurekebisha tabia.

Tathmini ya Elimu ya Kibinafsi - Una haki ya mtoto wako kufanyiwa **IEE** kwa gharama ya umma, ikiwa haukubaliani na tathmini ya utawala wa shule.

Mpango Binafsi wa Elimu (IEP) – Hati iliyo na huduma anazopokea mtoto aliye na ulemavu ambayo wazazi hukuza kwa kushirikiana na wahudumu wa shule angalau kila mwaka.

Timu ya IEP – Kundi la watu linalofanya uamuzi kuhusu utambulisho, tathmini, usajili na upeanaji wa elimu ya umma inayofaa bila malipo kwa mtoto aliye na ulemavu na wanaobuni, kukagua na kuangalia upya IEPs ya mtoto.

Mazingira Mbadala ya Muda wa Elimu (IAES) – Usajili tofauti na ule ulio kwenye IEP ya mtoto ambapo mtoto sharti aendelee kufikia mitaala ya jumla ya elimu na kupokea huduma zinazomwezesha kuendelea ili kufikia malengo yake ya IEP kila mwaka. Mtoto anayewekwa kwenye mazingira mbadala ya muda ya elimu kutokana na utovu wa nidhamu.

Sehemu ya B - Sehemu ya IDEA inayohusu huduma wanazopewa watoto walio na ulemavu wa miaka 3 hadi 21.

Sehemu ya C - Sehemu ya IDEA inayohusu huduma wanazopewa watoto wanapozaliwa hadi wanapofika umri wa miaka 3.

Maelezo ya Utambulisho (PII) – ni data yoyote inayoweza kumtambulisha mtu mahususi.

Huduma Husika – Usafiri na huduma za kuendeleza, kurekebisha na huduma zingine saidizi zinazohitajika kusaidia mtoto aliye na ulemavu kufaidika kutokana na elimu ya walio na ulemavu.

Siku ya Shule – Siku yoyote, ikijumuisha nusu siku ambayo wanafunzi huhudhuria shule ili kupata mafunzo. Siku ya shule ni sawa kwa kila watoto shuleni, ikijumuisha watoto walio na wasio na ulemavu.

SDCL – Sheria Iliyoandikwa ya South Dakota

SEA – Shirika la Elimu ya Kitaifa: Bodi ya elimu ya kitaifa au shirika lingine au afisa aliye na wajibu mkuu wa kusimamia shule za msingi na sekondari katika Taifa.

Elimu Kwa Watu Walio na Ulemavu – Mbinu mahususi ya kufunza, bila wazazi kulipa ada yoyote, ili kukidhi mahitaji ya kipekee ya mtoto aliye na ulemavu, ikijumuisha mafunzo ya darasani, nyumbani, hospitalini na katika mashirika na katika mipangilio mingine, na mbinu ya kufunza elimu ya michezo. Elimu kwa walemavu inajumuisha pia kila mojawapo ya yafuatayo: huduma zinazobaini matamshi, au huduma nyingine husika, ikiwa inachukuliwa kuwa elimu ya walio na ulemavu bali na kuwa huduma husika kwa mujibu wa Vigezo, mafunzo ya usafiri na elimu; na mafunzo ya ufundi.

Huduma za Mabadiliko – Aina mbalimbali ya shughuli zilizopangiwa mtoto aliye na ulemavu ambazo (1) zimebuniwa kuwa mchakato wa kutarajia matokea, yanayolenga kuboresha ufanisi wa mtoto aliye na ulemavu kimasomo na kiutendakazi ili kumuwezesha kutekeleza shughuli akiwa shuleni na hata baada ya shule, ikijumuisha masomo baada ya sekondari, masomo ya ufundi, ajira timilifu (ikijumuisha ajira saidizi), masomo endelevu na ya watu wazima, huduma kwa watu wazima, kujitegemea, au ushirikiano wa jumuiya; (2) inategemea mahitaji ya mtoto, ikiangalia nguvu na mapendeleo yake, na maslahi, na inajumuisha: njia ya kufunza; huduma husika; huduma za kijamii; ukuaji wa ajira na malengo mengine ya watu wazima baada ya shule; na panapohitajika, kupata maarifa ya kuishi kila siku na uwezo wa kutathmini utendakazi wa kiufundi.

Idara ya Elimu – Wawakilishi wa Kimkoa

Idara ya Elimu ya South Dakota
Mipango ya Elimu kwa Watu Walio na Ulemavu
800 Governors Drive
Pierre, SD 57501-2294
voice - (605) 773-3678
faksi - (605) 773-3782
<https://doe.sd.gov/sped/>

Watu wa Kuwasiliana nao ili Kupata Usaidizi Zaidi katika Kuelewa Haki Zako

Muungano wa Wazazi wa South Dakota
3701 W. 49th Street, Suite 102
Sioux Falls, SD 57106
1-800-640-4553
www.sdparent.org

Haki za Watu Walio na Ulemavu katika South Dakota
2520 East Franklin
Pierre, SD 57501
1-800-658-4782 (voice/TTY) au
(605) 224-8294
<https://drsdlaw.org/>